**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA UJENZI

# MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA BARA

# SEKTA YA UJENZI




DAR ES SALAAM
S.L.P 9423

01 Septemba, 2011.



Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal
**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



Mheshimiwa Mizengo Kayanza P. Pinda (Mb)
**Waziri Mkuu**



Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli (Mb)
**WAZIRI WA UJENZI**



Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb)
**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**



Balozi Herbert E. Mrango
**KATIBU MKUU**



Eng. Dkt. John S. Ndunguru
**NAIBU KATIBU MKUU**

**WAKURUGENZI, WAKUU WA VITENGO NA VIONGOZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA UJENZI MWAKA 2011**

i. **Wenyeviti wa Bodi**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | Tanroads | - | Abel Mwaisumo |
| b. | Wakala wa Ufundi na Umeme | - | Prof. Idrissa .B. Mshoro |
| c. | Wakala wa Majengo | - | Dr. K. Edward. W. Ngwale |
| d. | Baraza la Taifa la Ujenzi | - | Prof. Eng. Burton.M. Mwamila |
| e. | Mfuko wa Barabara | - | Dkt. James.M. Wanyancha |
| f. | Bodi ya Usajili wa Makandarasi | - | Eng. Consolata Ngimbwa |
| g. | Bodi ya Usajili wa Wahandisi | - | Prof. Ninatubu Lema |
| h. | Bodi ya Usajili Wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi | - | Arch. Dkt. Ambwene Mwakyusa |

ii. **Wakurugenzi na Wakuu Vitengo**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | Bibi Juliana Mwakitosi | - | Mkurugenzi wa Utawala & Rasilimali Watu |
| b. | Eng. Madeni Kipande | - | Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira |
| c. | Bibi Elizabeth Tagora | - | Mkurugenzi wa Mipango |
| d. | Eng. Alois Matei | - | Mkurugenzi Msaidizi wa Barabara Kuu |
| e. | Eng. Fintan Kilowoko | - | Mkurugenzi Msaidizi wa Barabara za Mikoa |
| f. | Eng. John M. Kassanda | - | Mkurugenzi Msaidizi Majengo ya Serikali |
| g. | Eng. Ngome Rajabu Ngome | - | Mkurugenzi Msaidizi Ufundi na Umeme |
| h. | Eng. Martin Ntemo | - | Mkuu wa Kitengo cha Habari |
| i. | Bw. Projest Pastori | - | Mhasibu Mkuu |
| j. | Bibi Nuru Mhando | - | Mkaguzi wa Ndani |
| k. | Bw. Michael Liwanda | - | Mkuu wa Kitengo cha manunuzi |
| l. | Bibi Veronica Najima | - | Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| m. | Steven Stivin Nchimbi | - | Mkuu wa Kitengo cha Mifumo ya Kompyuta |

iii. **Watendaji Wakuu Wa Taasisi na Wakala**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | Wakala wa Barabara | - | Eng. Patrick A. Mfugale |
| b. | Baraza la Taifa la Ujenzi | - | Eng. K.M.M.M. Msita |
| c. | Mfuko wa Barabara | - | Bw. Joseph Haule |
| d. | Wakala wa Ufundi Na Umeme (Kaimu) | - | Eng. Maselini B. Magesa |
| e. | Wakala wa Majengo | - | Eng. John A. Njau |
| f. | Kikosi cha Wajenzi | - | Eng. Dismas F. Mgani |

iv. **Wasajili wa Bodi**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | Bodi ya Usajili Wa Makandarasi | - | Eng. Boniface Muhegi |
| b. | Bodi ya Usajili wa Wahandisi | - | Eng.Steven Mlote |
| c. | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (Kaimu). | - | Qs Albert Munuo |

v. **Wakuu wa Vyuo**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | Chuo cha Ujenzi (Morogoro) | - | Eng. John Aly Mdee |
| b. | Chuo cha ATTI (Mbeya) | - | Eng. Emmanuel Raphael |

***N.B:*** ***Kutokana na Wizara ya Ujenzi kuundwa upya mwaka 2011 kutoka kwa iliyokuwa Wizara ya Miundombinu, nafasi nyingi za Wakurugenzi ni za kukaimu.***

## Yaliyomo:


1. UTANGULIZI ........................................................................ 1
2. DIRA NA DHAMIRA YA WIZARA ................................................ 1
3. MAJUKUMU YA WIZARA ............................................................ 1
4. MALENGO YA WIZARA ............................................................. 1
5. HISTORIA YA VIONGOZI WA WIZARA ....................................... 2
5.1.1. Mawaziri ........................................................................ 3
5.1.2. Naibu Mawaziri ............................................................... 3
5.1.3. Makatibu Wakuu ............................................................. 4
5.1.4. Naibu Makatibu Wakuu ................................................... 4
6. HALI YA BARABARA, NYUMBA ZA SERIKALI, HUDUMA ZA UFUNDI NA VIVUKO MWAKA 1961 .......................................... 6
6.1. Barabara .......................................................................... 6
6.2. Ufundi na Umeme ............................................................. 7
6.3. Nyumba za Serikali ........................................................... 7
7. MAFANIKIO YA MIAKA 50 YA UHURU KATIKA SEKTA YA UJENZI .......................................................................... 8
7.1. BARABARA ........................................................................ 8
7.1.1. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo: 1964 – 1969 ....................... 9
7.1.2. Mpango wa Pili wa Maendeleo: 1969 - 1974 .............................10
7.1.3. Miradi Mikubwa ya Barabara Katika Kipindi cha Miaka 50 ya Uhuru ..............................................................................13
7.1.4. Mradi Maalum wa Barabara (2000 hadi 2011) .........................14
7.1.5. Utekelezaji wa miradi ya barabara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ..........................................................................20
7.1.6. Miradi Mikubwa ya Madaraja ..................................................27
7.1.7. Miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. ..............................................................................27
7.1.8. Mradi wa mabasi yaendayo kasi (DART) (km 20.9): ...................28
7.1.9. Wakala wa Barabara Nchini ....................................................28
7.1.10. Mfuko wa Barabara ...............................................................32
7.2. UFUNDI NA UMEME ................................................................33
7.2.1. Wakala wa Ufundi na Umeme ..................................................37
7.3. WAKALA WA MAJENGO ............................................................41
7.3.1. Mafanikio ya Miaka Hamsini (50) ya Uhuru ..............................41
7.3.2. Viwanja/Mashamba ya Wakala wa Majengo (TBA) .....................45
7.3.3. Malengo na Mwelekeo kwa Wakati Ujao ...................................45
7.4. USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA ................................. 45
7.4.1. Mafanikio katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru .......................46
7.4.2. Menejimenti ya Usalama .........................................................46
7.4.3. Menejimenti ya Mazingira ........................................................47
7.4.4. Mipango ya Miaka ijayo ...........................................................48
7.5. SERA NA SHERIA ................................................................... 49

7.6. BARAZA LA TAIFA LA UJENZI (NCC) .......................................... 49
7.6.1. Mafanikio katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru......................50
7.7. BODI YA USAJILI WA WAHANDISI.......................................... 50
7.7.1. Mafanikio ya Bodi katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru .........50
7.8. BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI ..................................... 50
7.8.1. Mafanikio ya Bodi kwa kipindi cha miaka 50 ya Uhuru............50
7.9. BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI ......................................................... 51
7.9.1. Mafanikio ya Bodi kwa kipindi cha miaka 50 ya Uhuru............51
7.10. KIKOSI CHA UJENZI ............................................................. 51
7.10.1. Mafanikio ya Kikosi kwa kipindi cha miaka 50 ya Uhuru ..........52
7.11. CHUO CHA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA STAHILI YA NGUVUKAZI ........................................................................ 53
7.11.1. Mafanikio ya Chuo.................................................................53
7.12. CHUO CHA UJENZI MOROGORO ............................................ 53
7.12.1. Mafanikio ya Chuo.................................................................54
7.13. KITENGO CHA USHIRIKISHWAJI WA WANAWAKE KATIKA KAZI ZA BARABARA ............................................................... 54
7.13.1. Mafanikio ya Kitengo kwa Kipindi cha miaka 50 ya Uhuru........55
8. HITIMISHO ........................................................................... 56
9. MTANDAO WA BARABARA NCHINI.......................................... 58
10. VIONGOZI WALIOONGOZA NAFASI YA RAIS KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 KUANZIA MWAKA 1961................................... 66
11. VIONGOZI WALIOONGOZA NAFASI YA MAKAMU WA RAIS KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 KUANZIA MWAKA 1961I......... 67
12. VIONGOZI WALIOONGOZA NAFASI YA WAZIRI MKUU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 KUANZIA MWAKA 1961....................... 68

## 1. UTANGULIZI

Wizara ya Ujenzi, ikiwa sehemu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalo jukumu la kusimamia Sekta za Ujenzi ambayo ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

## 2. DIRA NA DHAMIRA YA WIZARA

Dira ya Wizara ni kuwa na: Barabara, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi zenye ubora wa kiwango cha juu, zenye gharama nafuu, zinazozingatia usalama na utunzaji wa mazingira.

Aidha, dhamira ya Wizara ni kuwa na: Barabara, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi ambazo ni salama, zinazotegemewa, zilizo na uwiano na ambazo zinakidhi mahitaji ya usafiri na uchukuzi katika kiwango bora kwa bei nafuu na zinazoendana na mikakati ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na zikiwaendelevu kiuchumi na kimazingira.

## 3. MAJUKUMU YA WIZARA

Wizara ya Ujenzi imekabidhiwa majukumu ya kusimamia ujenzi na matengenezo ya Barabara, Madaraja, Vivuko na Majengo ya Serikali na Masuala ya Ufundi ambayo yanahusisha Magari, Mitambo, Umeme na Elektroniki pamoja na shughuli za Uhandisi na Usanifu wa Ujenzi, Usalama wa Miundomninu na Mazingira; na uboreshaji wa Utendaji na Uendelezaji wa Watumishi wa Wizara, na Taasisi zinazosimamiwa kisera na Wizara.

Majukumu ya Wizara yamekuwa yakibadilika katika nyakati tofauti. Hata hivyo jukumu la msingi ambalo limekuwa likisimamiwa kwa kipindi chote cha miaka 50 ni usimamizi wa Sera, Sheria, Kanuni na miradi ya sekta ya Ujenzi na Usafirishaji. Wizara ya ujenzi ndiyo yenye dhamana ya kutoa miongozo (guidelines), vigezo (standards) na viwango (specifications) vya ubora katika sekta hii ikiwa ni pamoja na usimamizi wa usalama wa miundombinu inayoendana na eneo linalosimamiwa na wizara hii.

## 4. MALENGO YA WIZARA

Malengo ya Wizara ni pamoja na kuhakikisha kuwa miji yote mikuu ya mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwaka 2017/18 na kuendelea kusimamia wataalamu wa sekta (Wahandisi, Wahandisi Washauri, Makandarasi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi) kwa kutumia bodi husika ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi viwango. Aidha, Wizara itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia

sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya Ujenzi na inaendelea kushirikiana na taasisi husika katika kushughulikia masuala mtambuka kama vile kampeni za kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, uhifadhi wa mazingira, masuala ya jinsia na uendelezaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

## 5. HISTORIA YA VIONGOZI WA WIZARA

Mwaka 2011, Tanzania inasheherekea miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika wakati ambapo Wizara ya Ujenzi inaongozwa na Waziri Mheshmiwa, Dkt. John Pombe Magufuli Mbunge wa jimbo la Chato (CCM), na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt.Harrison L. Mwakyembe Mbunge wa jimbo la Kyela (CCM). Katibu Mkuu ni Balozi Herbert Eliadi Mrango ambaye anasaidiwa na Naibu Katibu Mkuu, Eng. Dkt. John Ndunguru.



Kuanzia mwaka 1961, Viongozi Wakuu walioongoza Wizara ya Ujenzi ni kama ifuatavyo:

### *5.1.1. Mawaziri*

| | | |
|---|---|---|
| 1961 – 1963 | Bw. Amir Jamal | Mawasiliano, Umeme na Ujenzi |
| 1963 – 1965 | Bw. George Kahama | Mawasiliano, Umeme na Ujenzi |
| 1965 – 1975 | Bw. Job Lusinde | Mawasiliano, Kazi na Ujenzi |
| 1975 – 1975 | Bw. L. A. Sazia | Mawasiliano, Kazi na Ujenzi |
| 1976 – 1976 | Bw. Alfred Tandau | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1976 – 1982 | Bw. Samwel Sitta | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1982 – 1984 | Bw. John S. Malecela | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1983 – 1985 | Bw. Gutram Itatiro | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1985 – 1988 | Bw. Mustafa Nyang'anyi | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1988 – 1989 | Bw. Steven Kibona | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1989 – 1990 | Bw. Dkt. Pius Ng'wandu | Ujenzi |
| 1990 – 1995 | Bw. Nalaila Kiula | Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 1995 – 2000 | Bibi Anna Abdallah | Ujenzi |
| 2000 – 2005 | Bw. John P. Magufuli | Ujenzi |
| 2005 – 2006 | Bw. Basil Mramba | Miundombinu |
| 2006 – 2008 | Bw. Andrew Chenge | Miundombinu |
| 2008 – 2010 | Bw. Shukuru Kawambwa | Miundombinu |
| Kuanzia 2010 | Bw. Dkt. John P. Magufuli | Ujenzi |

### *5.1.2. Naibu Mawaziri*

| | | |
|---|---|---|
| 1963 - 1964 | Chief Erasto Mang'enya | Mawasiliano, Umeme na Ujenzi |
| 1964 - 1965 | Bw. John Mhavile | Mawasiliano, Umeme na Ujenzi |
| 1965 - 1967 | Bw. Omar Muhaji | Mawasiliano, Umeme na Ujenzi |
| 1967 - 1968 | Bw. Fulgence Mponji | Mawasiliano, Kazi na Ujenzi |
| 1968 - 1969 | Bw. Edward Sokoine | Mawasiliano, Kazi na Ujenzi |
| 1969 - 1973 | Bw. Richard Wambura | Mawasiliano, Kazi na Ujenzi |
| 1973 - 1974 | Bw. Robert Ng'itu | Mawasiliano, Kazi na Ujenzi |
| 1974 - 1978 | Bw. Mustafa Nyang'anyi | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1978 - 1984 | Bw. Edger Majogo | Mawasiliano na Ujenzi |

| | | |
|---|---|---|
| 1984 - 1987 | Bw. Arcado Ntagazwa | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1987 - 1991 | Bw. Edger Majogo | Mawasiliano na Ujenzi |
| 1991 – 1993 | Bw. Meja Sigellah Nswima | Ujenzi |
| 1993 - 1995 | Bw. Gerald Ghachocha | Ujenzi/Mawasiliano/Uch. |
| 1995 - 2000 | Bw. John P. Magufuli | Ujenzi |
| 2000 - 2005 | Bw. Hamza Mwenegoha | Ujenzi |
| 2005 - 2006 | Bw. Dkt. Makongoro Mahanga | Miundombinu |
| 2006 - 2008 | Bw. Dkt. Makongoro Mahanga | Miundombinu |
| 2008 - 2010 | Bw. Hezekiah Chibulunje | Miundombinu |
| Kuanzia 2010 | Bw. Dkt. Harisson Mwakyembe | Ujenzi |

### *5.1.3. Makatibu Wakuu*

| | |
|---|---|
| 1962 | Bw. Frederick Burengelo |
| 1962 – 1965 | Bw. Juma Maggid |
| 1965 - 1968 | Bw. Ainamansa Mbuya |
| 1968 - 1978 | Bw. J. Sepeku |
| 1978 - 1979 | Bw. Daniel Mloka |
| 1979 - 1980 | Bw. Odira Ongara |
| 1980 - 1983 | Bw. Richard Juma |
| 1984 - 1987 | Bw. Odira Ongara |
| 1987 - 1989 | Bw. Paul Mkanga |
| 1989 - 1990 | Bw. Felician Mujuni |
| 1990 - 1995 | Bw. Eng. Dkt.George Mlingwa |
| 1995 - 1998 | Bw. Abdi Mshangama |
| 1998 - 2002 | Bw. Solomon Odunga |
| 2002 - 2006 | Bw. Eng. John Kijazi |
| 2006 - 2008 | Bw. Dkt. Ernos Bukuku |
| 2008 - 2010 | Bw. Eng. Omar Chambo |
| Kuanzia 2011 | Bw. Herbert E. Mrango |

### *5.1.4. Naibu Makatibu Wakuu*

| | |
|---|---|
| 2006 - 2008 | Bw. Eng. Omar Chambo |
| 2008 - 2009 | Bibi Joyce Mapunjo |
| 2010 - 2011 | Bw. Herbert E. Mrango |
| Kuanzia 2011 | Bw. Eng. Dkt. John S. Ndunguru |

## MAWAZIRI WALIOONGOZA SEKTA YA UJENZI (1961 – 2011)



Amir Jamal
1961 - 1963



Sir George Kahama
1963 - 1965



Job Lusinde
1965 - 1975



L.A. Sazia
1975 - 1975



Alfred Tandau
1976 - 1976



Samwel J. Sitta
1976 - 1982



John S. Malecela
1982 - 1984



Gutram Itatiro
1983 - 1985



Mustafa Nyang'anyi
1985 - 1988



Steven Kibona
1988 - 1989



Dkt. Pius Ng'wandu
1989 - 1990



Nalaila Kiula
1990 - 1995



Anna Abdallah
1995 - 2000



John P. Magufuli
2000 – 2005



Basil Mramba
2005 - 2006



Andrew Chenge
2006 - 2008



Dkt. Shukuru Kawambwa
2008 - 2010



Dkt. John P. Magufuli
Kuanzia 2010


# 6. HALI YA BARABARA, NYUMBA ZA SERIKALI, HUDUMA ZA UFUNDI NA VIVUKO MWAKA 1961

Wakati tunapata Uhuru mwaka 1961, hali ya Barabara, Nyumba za Serikali, Ufundi na Vivuko ilikuwa kama ifuatavyo;

## 6.1. Barabara

Mwaka 1961 wakati wa Uhuru, nchi ya Tanganyika, ilikuwa na ukubwa wa maili za mraba 360,000 (921,600 $km^2$) na watu 9,540,000, wengi wao wakijishughulisha na kilimo, ufugaji na uvuvi sehemu za vijijini.

Wakati huo wa Uhuru mtandao wa barabara ulikuwa na jumla ya kilometa 33,600 zilizojumuisha kilometa16,000 zilizokuwa zikitambuliwa kama Barabara Kuu za Nchi na za Kawaida (Territorial Main and Local Main Roads) na kilometa 17,600 zikiwa ni Barabara za Wilaya (District Roads):



Barabara ya Dodoma – Singida eneo la Saranda mwaka 1969

## 6.2. Ufundi na Umeme

Idara ya Ufundi na Umeme (Electrical and Mechanical – E&M) ilianza tangu mwaka 1961 chini ya Idara ya Kazi za Umma (Public Works Department – PWD)

i. Karakana za Ufundi

Wakati tunapata Uhuru kulikuwepo na Karakana Kuu ya *M. T. Depot* Dar es Salaam pamoja na karakana nyingine nane (8) katika mikoa ya Dodoma, Tanga, Tabora, Morogoro, Mwanza, Mbeya, Mtwara na Iringa kwa ajili ya matengenezo ya magari ya Serikali. Wakati huo kulikuwa na magari yaliyosajiliwa yapatayo 38,000 yakiwa ni magari ya Serikali na watu binafsi.. Aidha, kulikuwepo na karakana ya mitambo mikubwa (Heavy Plant) mjini Morogoro kwa ajili ya matengenezo ya mitambo mikubwa iliyokuwa ikihusika na matengenezo ya barabara na miundombinu ya maji.

ii. Vivuko

Wakati nchi yetu inapata Uhuru mwaka 1961 hapakuwa na kivuko hata kimoja kinachojiendesha chenyewe. Vivuko vichache vilivyokuwepo vilikuwa ni vya kuvutwa kwa kamba. Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na vivuko vya aina hiyo ni pamoja na; Utete (Mto Rufiji), Kigongoni (Mto Ruvu), Kisauke (Mto Wami), Kirumi (Mto Kirumi) na Ruhuhu (Mto Ruhuhu).

## 6.3. Nyumba za Serikali

Wakati Tanganyika inapata Uhuru mwaka 1961, Serikali ilirithi kutoka kwa utawala wa Wakoloni nyumba zipatazo 6,000 ambazo zilikuwa zimegawanyika katika makundi mawili; nyumba za Daraja A walizokuwa wanaishi watumishi wa ngazi za juu (wengi wao wakiwa wazungu) ambazo zilikuwa katika maeneo maalum (prime areas) na nyumba za Daraja B zilizokuwa zinatumiwa na watumishi waandamizi Serikalini (waafrika).

Idadi hiyo ndogo ya nyumba za Serikali ilikidhi kiasi cha asilimia tatu (3%) tu ya watumishi wa Serikali. Idadi ya nyumba za kuishi watumishi wa Serikali ambazo zilikuwa chini ya usimamizi wa Idara Kuu ya Utumishi haikuongezeka kwa kipindi kirefu bali zilizokuwepo ziliendelea kufanyiwa ukarabati mdogo mdogo.

Kutokana na idadi ya watumishi Serikalini kuongezeka kadri ukubwa wa Serikali ulivyokuwa unaongezeka, tatizo la uhaba wa makazi ya kudumu kwa watumishi wa Serikali liliongezeka. Kutokana na changamoto hiyo Serikali iliunda tume mbalimbali zilizotoa ushauri wa kitaalamu kuhusu namna bora ya kupunguza tatizo hili.

Baadhi ya tume hizo ni;

Tume ya ADU mwaka 1963
Tume ya Nsekela ya mwaka 1975
Tume ya Mramba mwaka 1984

Tume hizo zote zilipendekeza kuwa Serikali iondokane na gharama kubwa ya kumiliki na kukarabati nyumba hivyo, kupendekeza kuanzishwa kwa chombo kinachojitegemea kitakachoshughulikia suala la ujenzi wa nyumba za kuishi watumishi.

Kwa kutumia Sheria Na. 30 ya mwaka 1997 ya Wakala za Serikali (Executive Agencies Act No. 30/1997), Serikali ilianzisha Wakala wa Majengo ya Serikali tarehe 17 Mei, 2002.

## 7. MAFANIKIO YA MIAKA 50 YA UHURU KATIKA SEKTA YA UJENZI

Katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara kuanzia mwaka 1961 hadi 2011 tumepata mafanikio makubwa katika Sekta ya Ujenzi kwenye maeneo ya Barabara, Ufundi na Umeme, Vivuko na Nyumba. Aidha, kumekuwa na mabadiliko mbali mbali ya kisera yaliyoendana na utungwaji wa sheria kadhaa.

Mafanikio haya katika Sekta ya Ujenzi yamefanikisha kukua kwa mtandao wa barabara na hasa ujenzi wa barabara za lami, matengenezo na ukarabati wa barabara, madaraja, magari na vivuko na nyumba za Serikali yamekwenda sambamba na ongezeko la bajeti ya kutoka Shilingi bilioni 2.1 mwaka 1962/63 hadi kufikia Shilingi trilioni 1.496 mwaka 2011/2012.

### 7.1. BARABARA

Tangu Uhuru mwaka 1961 hadi 2011, Tanzania Bara imepata mafanikio makubwa katika sekta ya barabara, sekta ambayo ina mchango muhimu katika kuinua uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mtandao wa barabara nchini umekuwa ukiboreshwa na kuongezeka kwa kuweka mkazo katika ujenzi na ukarabati wa Barabara Kuu, Barabara za Mikoa, Barabara za Wilaya na Madaraja kwa lengo la kuleta uhakika na nafuu ya usafiri na usafirishaji nchini. Aidha, kipaumbele kimetolewa katika kutunza, kutengeneza na kukarabati barabara kupitia mipango na miradi mbali mbali iliyoandaliwa.

Juhudi hizi za Serikali zimewezesha mtandao wa barabara kupanda kutoka kilometa 33,600 zilizokuwepo mwaka 1961 hadi kufikia kilometa 86,472 mwaka 2011 (ramani zinazoonyesha mtandao unaoonyesha Barabara Kuu

na za mikoa kwa kila mkoa zimeonyeshwa katika Sura ya Na. 8). Aidha mtandao wa barabara za lami umeongezeka kutoka kilometa 1,360 hadi kufikia kilometa 6,500 wakati sasa (2011) zaidi ya kilometa 11,154 ziko katika hatua mbali mbali za ujenzi kwa kiwango cha lami.

### *7.1.1. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo: 1964 – 1969.*

Ili kufanikisha malengo ya kiuchumi kitaifa, mwaka 1964 Serikali ilitayarisha mpango wa kwanza wa ujenzi na ukarabati wa barabara.

Mpango wa maendeleo wa miaka mitano wa mwaka 1964 hadi 1969 ulilenga kufanya yafuatayo:

i. Barabara Kuu (Trunk and Major Links) kuendelezwa na kuboreshwa kwa kuzingatia wingi na uzito wa magari

ii. Barabara zilizojulikana kama 'Major Feeder Roads' kuboreshwa au kujengwa kwa kuzingatia vigezo vya kurahisisha usafirishaji wa kiuchumi pale inapodhihirika kuna ongezeko la mazao yanayozalishwa na bidhaa nyingine.

iii. Barabara zilizojulikana kama 'Minor Feeder Roads' kuboreshwa au kujengwa kwa lengo la kuhakikisha zinaunganishwa na kupitika katika maeneo yaliyothibitika kuwa na maendeleo.

iv. Kuhakikisha kila mradi unafanyiwa upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kutekelezwa.

Kwa kulinganisha na mpango wa miaka mitatu ya kwanza (1961 hadi 1963) mpango huu ulikuwa na sifa mbili kuu:

i. Bajeti ya maendeleo iliongezwa kwa asilimia sabini na tano (75%) kwa kila mwaka ikilinganishwa na mpango wa miaka mitatu

ii. Kuliwekwa mkazo mkubwa zaidi katika bababara za vijijini (feeder roads).

Mafanikio ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo (1964 – 1969) yalikuwa ni kujengwa kwa kiwango cha lami vipande vifuatavyo vya Barabara Kuu ya Dar es Salaam – Moshi – Arusha – Namanga:

i. Chalinze – Segera

ii. Mkumbara – Kisangiro

Kujengwa kwa kiwango cha changarawe (engineered gravel standard) Barabara Kuu zifuatazo:

i. Mtwara – Mingoyo – Masasi

ii. Songea – Njombe (kipande cha milimani)

Kujengwa kwa Barabara Kuu za Ndani (Major Feeder Roads) zifuatazo:

i. Uyole – Itungi Port (Lami)

ii. Kolandoto – Bariadi (Changarawe)

iii. Bunda – Nansio (Changarawe)

### *7.1.2. Mpango wa Pili wa Maendeleo: 1969 - 1974*

Mpango ulikuwa na malengo yaliyoandaliwa kwa kuzingatia maono ya muda mfupi (hadi mwaka 1974), muda wa kati (1980 na 1985) na wa muda mrefu (mwaka 1990) ili kuweza kuongoza utendaji na kuruhusu kurejewa kwa mipango kwa kuzingatia changamoto zilizotarajiwa kujitokeza pamoja na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Aidha, lengo lilikuwa kwamba ifikapo mwaka 1990 Mikoa yote iwe imeunganishwa kwa barabara zinazopitika wakati wote.

Kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha vipaumbele vilikubalika kama ifuatavyo:

i. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa TanZam Highway kilometa 496,

ii. Ujenzi wa barabara nyingine kwenye mtandao wa Barabara Kuu za Nchi kilometa 890,

iii. Ujenzi wa kuboresha uwezo wa njia kwa kiwango kinachokubalika ili kupitika muda wote barabara nyingine zilizo kwenye mtandao wa 'Major Link Roads' kilometa 1203,

iv. Kuweka Msukumo mkubwa kwenye 'Minor Feeder Roads' ikilinganishwa na 'Major Feeder Roads' katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa kilimo, na

v. Kuchagua miradi kwa kuzingatia matakwa ya kukua kwa uchumi

Mafanikio ya Mpango wa Pili wa Maendeleo 1969 – 1974 yalikuwa ni kupewa majina rasmi ya utambulisho wa barabara kama ifuatavyo;

| Jina | Mwelekeo |
|---|---|
| **T1** | Kenya Border – Tanga – Segera – Chalinze – Mtwara (kupitia 'Stiegler's Gorge – Nachingwea – Nanganga – Mingoyo' au 'Dar es Salam – Kibiti – Mohoro – Lindi') |
| **T2** | Kenya Border (Namanga) – Arusha – Makuyuni – Babati – Dodoma – Iringa |
| **T3** | Uganda Border – Bukoba – Biharamulo – Nyakanazi – Kasulu – Mpanda – Sumbawanga – Tunduma. |
| **T4** | Segera – Korogwe – Moshi – Arusha – Makuyuni – Maswa – Mwanza – Usagara – Geita – Biharamulo – Rwanda Border. |
| **T5** | Morogoro – Dodoma – Singida – Nzega – Shinyanga – Usagara – Mwanza |
| **T6** | Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Iringa – Makambako – Mbeya – Tunduma |
| **T7** | Mtwara – Masasi – Tunduru – Songea – Njombe – Makambako |


Aidha Ramani Na 2 (Uk 12) inafafanua utekelezaji wa miradi husika.





Rais wa Awamu ya Kwanza Mwalimu Julius K. Nyerere akiwa na Rais wa Rwanda Mhe. George Kaibanda wakifungua rasmi Daraja la Rusumo mwaka 1972. Daraja hili liko katika mpaka wa Tanzania na Rwanda

**Kielelezo Ramani 2:**
**Maono ya mtandao wa barabara mwaka 1974**



### *7.1.3. Miradi Mikubwa ya Barabara Katika Kipindi cha Miaka 50 ya Uhuru*

Kwa kutumia fedha za ndani na kwa kushirikiana na washirika mbali mbali wa maendeleo wa ndani na nje, Tanzania Bara imeweza kutekeleza miradi mbali mbali ya ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja kama ifuatavyo;

i. Mradi wa Kwanza wa Barabara Kuu (1st Highway Project) 1962 hadi 1968.

ii. Mradi wa Pili wa Barabara Kuu (Second Highway Project) 1969 hadi 1971

iii. Mradi wa tatu wa barabara Kuu (Third Highway Project) 1971 hadi 1974)

iv. Mradi wa Nne wa Barabara Kuu (4th Highway Project) 1974 hadi 1982

v. Mradi wa Tano wa Barabara Kuu (5th Highway Project) 1980 hadi 1985

vi. Mradi wa Sita wa Barabara Kuu (6th Highway Project) 1986 hadi 1994

vii. Miradi ya Barabara za Mazao

viii. Mradi wa uwiano wa barabara nchini - awamu ya kwanza (Integrated Road Project II – IRP - I) 1991 - 1999

ix. Mradi wa Uwiano wa Barabara nchini - awamu ya pili (Integrated Road Project II – IRP - II)

x. Mradi wa Kuendeleza Ukanda wa Kati wa Usafirishaji (Central Transport Corridor Project) 2004 hadi 2010

Katika kutekeleza miradi hii, barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami ni chache kwani miradi mingi ilijengwa kwa kiwango cha changarawe.

Baadhi ya miradi iliyotekelezwa kwa kiwango cha lami ni kama ifuatavyo;

Dar es Salaam – Morogoro, Morogoro – Dodoma, Singida – Shelui – Nzega, Nzega – Tinde – Shinyanga – Mwanza Border, Tinde – Isaka, Isaka – Lusahunga - Lusumo, Mwanza – Musoma – Sirari, Chalinze – Segera – Tanga, Segera – Moshi – Arusha – Namanga, Arusha – Makuyuni – Minjingu, Makuyuni – Ngorongoro, Morogoro – Iringa – Mbeya - Tunduma, Makambako – Songea, Mtwara – Mingoyo – Masasi.

Aidha madaraja makubwa ya Mkapa (Pwani), Kirumi(Mara), Mpiji (Pwani/DSM), madaraja ya Tanzam na Tunduma – Sumbwanga na Tanga – Horohoro n.k.

Tangu 1961 hadi 2011 tunapoadhimisha miaka 50 ya Uhuru, kuna jumla ya madaraja 4,880 yaliyokwisha jengwa.

### *7.1.4. Mradi Maalum wa Barabara (2000 hadi 2011)*

Mradi Maalum wa Barabara uliendana na ujenzi wa barabara na madaraja kwa kutumia fedha za ndani. Hivyo, ili kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara za lami, mwaka 2001 Serikali iliamua kuanzisha mradi maalum wa kujenga barabara kwa kutumia fedha zake yenyewe. Kiasi cha Shilingi bilioni 1.84 kilikuwa kikitengwa kila mwezi kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo;

i. Barabara ya kuunganisha Dar es Salaam na mikoa ya kusini.

   Katika mradi huu sehemu za Somanga – Matandu (km 33), Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95) na Mbwemkuru – Mingoyo (km 95) zilijengwa kwa kiwango cha lami na kukamilika.

ii. Barabara ya kuunganisha Dar es Salaam, mikoa ya kati na kanda ya ziwa.

   Katika mradi huu sehemu za; Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 120), Geita – Usagara (km 90), Dodoma – Manyoni (km 127) na Manyoni – Singida (km 118) zilijengwa kwa kiwango cha lami na na kukamilika.

iii. Kagoma – Biharamulo - Lusahunga (km 154)

   Kazi zilianza tarehe 16 septemba 2009 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012 kwa gharama ya shilingi bilioni 191.46.

iv. Barabara za Kahama Mjini (km 5)

   Ujenzi wa kilometa 1.5 za mwanzo umekamilika mwezi Machi 2011 kwa gharama ya shilingi milioni 760.

v. Barabara ya Uwanja wa Ndege – Pugu – Kisarawe – Mpuyani (km 25.5)

   Ujenzi kwa sehemu ya Uwanja wa Ndege – Pugu na sehemu ya Pugu – Kisarawe Mpuyani ulikamilika mwaka 2007

vi. Barabara ya TAMCO – Tumbi – Picha ya Ndege (km )

Ujenzi ulikamilika mwaka 2002

vii. Barabara ya Kyaka - Bugene (km 59.1)

Kazi zilianza mwaka 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 64.96.

viii. Barabara ya Kyabakari – Butiama (km 12)

Ujenzi ulikamilika mwaka 2005.

ix. Barabara ya Bariadi - Lamadi (km 71.8)

Kazi zilianza tarehe 8 Julai 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 67.41.

x. Barabara ya Sumbawanga - Matai-Kasanga Port (km 112)

Kazi zilianza tarehe 13 Januari, 2010 na zinafanyika kwa njia ya kusanifu na kujenga (Design & Build). Kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013 kwa gharama ya shilingi bilioni 133.29 .

xi. Barabara ya Sumbawanga-Kanyani-Nyakanazi (km 829).

Mradi huu imegawanywa katika sehemu nne kama ifuatavyo:-

*Sumbawanga - Kanazi (km 75)*

Kazi zilianza tarehe 16 Desemba 2009 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Gharama ni shilingi bilioni 78.84 .

*Kanazi – Kizi - Kibaoni (km 76.6)*

Kazi zilianza tarehe 16 Desemba 2009 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Gharama ni shilingi bilioni 82.84 .

*Kizi – Sitalike - Mpanda (km 95)*

Usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa kutumia fedha za ndani.

*Mpanda – Uvinza – Kanyani - Nyakanazi (km 582.4)*

Usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa kutumia fedha za ndani.

xii. Barabara ya Marangu - Rombo Mkuu na Mwika - Kilacha (km 34)

Kazi zimekamilika mwaka 2011 kwa gharama ya shilingi bilioni 25.1.

xiii. Rombo Mkuu – Tarakea (km 32)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2010

xiv. Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2008

xv. Barabara ya Kwa Sadala-Masama (km 12.5)

Kazi zilianza tarehe 10 Machi 2010 na ujenzi unaendelea. Kazi zinatarajiwa kukamilika katika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 5.34 fedha za ndani.

xvi. Kibosho Shine – Kwa Rafael - International School (km 43)

Kazi zilianza tarehe 2 Machi 2010 na ujenzi unaendelea. Kazi zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 8.93 fedha za ndani.

xvii. Barabara ya Rau Madukani – Mawela - Uru Njari (km 12.5)

Kazi zilianza tarehe 2 Machi 2010. Ujenzi unaendelea na kazi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 4.88 fedha za ndani.

xviii. Barabara ya Kilua Nduoni - Marangu Mtoni (km 31.5)

Kazi zilianza tarehe 2 Machi 2010. Ujenzi unaendelea na kazi zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 9.10 fedha za ndani.

xix. Barabara ya Handeni - Mkata (km 54)

Kazi zilianza tarehe 28 Desemba, 2009 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 17 Novemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 57.34.

xx. Korogwe – Handeni (km 65)

Kazi zilianza mwaka 2009 na zinatarajiwa kukamilika mwaka kwa gharama ya shilingi bilioni 63.199

xxi. Barabara ya Mziha-Turiani-Magole (km 84.6).

Mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

*Magole – Turiani (km 48)*

Kazi zilianza tarehe 3 Machi, 2010 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 2 June 2012. Gharama ni shilingi bilioni 48.2.

*Turiani – Mziha (km 36.6)*

Usanifu umekamilika kwa kutumia fedha za ndani.

xxii. Barabara ya Dumila – Kilosa (km 63)

Mradi umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

*Dumila - Ludewa (km 45)*

Kazi zilianza tarehe 1 Februari 2009 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 10 Februari 2012. Gharama ni shilingi bilioni 41.93 .

*Ludewa - Kilosa (km 18)*

Usanifu umekamilika.

xxiii. Barabara ya Mbeya-Chunya-Makongorosi (km 115).

Mradi huu unagharamiwa kwa . Utekelezaji wake umegawanywa katika sehemu tatu kama ifuatavyo:

*Mbeya - Lwanjilo (km 36)*

Mkataba mpya ulisainiwa mwezi Desemba 2010 baada ya Mkandarasi wa awali (Kundan Singh) kushindwa kazi na kufukuzwa.

*Lwanjilo - Chunya (km 36)*

Kazi zilianza tarehe 5 Agosti, 2009 zinatarajiwa kukamilika tarehe 4 Novemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 40.28.

*Chunya - Makongorosi (km 43)*

Usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika.

xxiv. Barabara ya Ndundu-Somanga (km 60).

Kazi zilianza tarehe 15 Julai, 2008 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 58.82

xxv. Barabara ya Masasi - Mangaka (km 55.1).

Kazi zilianza tarehe 9 Desemba 2009 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 21.62 fedha za msaada toka Serikali ya Japan kupitia JICA.

xxvi. Barabara ya Bagamoyo (Makofia) - Msata (km 64).

Kazi zilianza tarehe 11 Agosti 2010 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 10 Agosti 2012 kwa gharama ya shilingi bilioni 89.61.

xxvii. Barabara ya Nzega - Tabora (km 115).

Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

*Nzega - Puge (km 56.1)*

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010. Kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Oktoba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 66.36.

*Puge - Tabora (km 58.8)*

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Oktoba 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 62.74.

xxviii. Manyoni – Itigi - Tabora (km 264).

Mradi huu utekelezaji wake umegawanywa katika sehemu tatu kama ifuatavyo;

*Tabora - Nyahua (km 85)*

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Gharama ni shilingi bilioni 93.41 .

*Manyoni – Itigi - Chaya (km 89.4)*

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa mwaka 2013. Gharama ni shilingi bilioni 109.64

*Chaya – Nyahua (km 90)*

Sehemu hii usanifu wake kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika.

xxix. Tabora - Urambo (km 94).

Mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo

*Tabora - Ndono (km 42):*

Mkataba ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Julai 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 51.35

*Ndono - Urambo (km 52)*

Mkataba ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Julai 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 59.77.

xxx. Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127)

Ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika mwaka 2009

xxxi. Barabara za Manyoni – Isuna (km 54)

Ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika mwaka 2011

xxxii. Barabara ya Isuna – Singida (km 65)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2008

xxxiii. Barabara ya Geita – Buzirayombo (km 120)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2008

xxxiv. Barabara ya Buzirayombo – Kyamyorwa (km 100)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2008

xxxv. Barabara ya TMJ - Monduli (km 14)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1999

xxxvi. Geita – Sengerema – Usagara (km 90)

Ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika mwaka 2010

xxxvii. Kigoma - kidahwe (km 36)

Ujenzi kwa kiwango cha lami zimekamilika mwaka 2010.

xxxviii. Mwandiga – Manyovu (km 60)

Ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika mwaka 2010.

xxxix. Barabara ya Dodoma – Babati (km 261).

Utekelezaji umegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

*Dodoma - Mayamaya (km 43.6)*

Mkataba wa ujenzi umesainiwa mwezi Mei 2010 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Gharama ni shilingi bilioni 40.61

.

*Bonga - Babati (km 19.2)*

Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 31 Mei 2010 na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwaka 2012 kwa gharama za shilingi bilioni 19.69 fedha za ndani.

xl. Barabara ya Musoma - Mwanza/Mara Border (km 85.5)

Ujenzi ulianza mwaka 2010 na unatarajiwa kukamilika 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 85.368.

xli. Barabara ya Nangurukuru - Kilwa (km 30)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1994

xlii. Barabara ya Sam Nujoma (km 4)

Ujenzi wa kuipanua kuwa njia nne ulikamilika mwaka 2008 kwa gharama ya shilingi bilioni 13.563

xliii. Barabara za Jijini Dar es Salaam (km 65)

Barabara nyingi za Jijini Dar es Salaam zilijengwa miaka ya 70 na zimekuwa zikifanyiwa matengenezo makubwa kwa vipindi tofauti. Barabara hizo ni Kongowe – Mjimwema (km 20), Tabata – Kinyerezi – Ukonga (km 14), Kigamboni – Mjimwema – Nafco Farm, Barabara ya Uhuru, Barabara ya Nyerere (km 12.5), Sokoine Drive, Old Bagamoyo,Bananaa – Kitunda, Mbagala – Msongola

xliv. Barabara zilizojengwa kwa Otta Seal

Barabara za Otta Seal ziko katika mikoa mbalimbali kama vile Dodoma, Kagera, Dar es Salaam n.k

### *7.1.5. Utekelezaji wa miradi ya barabara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo*

i. Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Iringa (km 530)

ii. Barabara ya Iringa – Mafinga – Makambako – Mbeya – Tunduma (km 403)

iii. Barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara sehemu ya Mikumi – Kidatu (km 35)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1998 kwa fedha za msaada wa SDC

iv. Barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara sehemu ya Kiberege – Ziginali (km 10)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2006 kwa fedha za msaada wa SDC

v. Barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara sehemu ya Kibaoni – Ifakara Mjini (km 7)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2008 kwa fedha za msaada wa SDC

vi. Barabara ya Msamvu – Morogoro (km 3.1)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2000 kwa fedha za msaada wa SDC

vii. Barabara ya Makambako – Songea (km 295)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1985

viii. Barabara ya Songea – Peramiho (km 20)

ix. Barabara ya Morogoro – Dodoma (km 259)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1978

x. Barabara ya Singida – Shelui (km 110)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2008

xi. Barabara ya Shelui – Nzega (km 112)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2005 kwa fedha za mkopo wa ADB

xii. Barabara ya Nzega – Tinde – Shinyanga – Ilula (km 138.5)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2007 kwa fedha za EU

xiii. Barabara ya Mwanza – Magogo River – Ilula (km 102)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1998.

xiv. Barabara ya Mtukura – Bukoba – Kagoma (km 139)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2005 kwa fedha za mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika

xv. Barabara ya Tinde – Isaka (km 30.5)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2007 kwa fedha za EU

xvi. Barabara ya Isaka – Lusahunga – Rusumo (km 332)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1994

Ukarabati wa Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 242).

Mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

*Isaka - Ushirombo (km 132)*

Kazi zilianza tarehe 18 Februari 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013 kwa gharama ya shilingi bilioni 145.34 fedha kutoka Jumuia ya Nchi za Ulaya (European Union).

*Ushirombo-Lusahunga (km 110)*

Kazi zilianza tarehe 18 Februari 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012 kwa gharama ya shilingi bilioni 114.56 kutoka Jumuia ya Nchi za Ulaya (EU).

xvii. Barabara ya Tunduma - Sumbawanga (km 231)

Mradi huu unagharamiwa na fedha za MCC na umegawanyika katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

*Tunduma - Ikana (km 63.7):*

Kazi zilianza tarehe 22 Septemba 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Gharama ni shilingi bilioni 82.52

*Ikana - Laela (km 64.2)*

Kazi zilianza tarehe 17 Septemba 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Gharama ni shilingi bilioni 76.1.

*Laela - Sumbawanga (km 95.1)*

Kazi zilianza tarehe 1 Aprili 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Gharama ni shilingi bilioni 130.1.

xviii. Barabara ya Tanga - Horohoro (km 65)

Ujenzi unaendelea kwa fedha za MCC na unatarajiwa kukamilika mwaka 2012.

xix. Barabara ya Mandela (km 16.8).

Kazi zilianza tarehe 1 Oktoba 2007 na zimekamilika tarehe 30 Juni 2011 kwa gharama ni shilingi bilioni 41.22 fedha za msaada toka EU.

xx. Ukarabati wa Barabara ya TANZAM sehemu ya Msimba – Ikokoto – Mafinga (km 219)

Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Denmark kupitia DANIDA. Utekelezaji umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

*Msimba-Ruaha - Mbuyuni/Ikokoto - Mafinga (km 149.6)*

Kazi za ukarabati zinatarajiwa kukamilika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 127.7.

*Iringa - Mafinga (km 69.4)*

Kazi zilianza mwaka 2011 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2014.

xxi. Barabara ya Arusha - Minjingu (km 104)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika kwenye miaka ya sabini. Aidha, kazi za ukarabati zitaanza mwaka 2011 na ukarabati unatarajiwa kukamilika mwaka 2014 kwa kugharamiwa na fedha za mkopo toka Benki ya Dunia.Jumla ya shilingi bilioni 78 zitatumika

xxii. Barabara ya Minjingu – Babati - Singida (km 223.5).

Mradi huu unagharamiwa na Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu kama ifuatavyo:

*Singida - Kateshi (km 65.1)*

Kazi zilianza tarehe 11 Machi, 2009 na zinatarajiwa kukamilika Septemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 51.63.

*Kateshi - Dareda (km 73.8)*

Kazi zilianza tarehe 11 Machi, 2009 na zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa 2011. Gharama ni shilingi bilioni 64.14

*Dareda – Babati - Minjingu (km 84.6)*

Kazi zilianza tarehe 11 Machi, 2009 na zimefikia asilimia 75 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 10 Machi, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 84.92. Barabara ya Korogwe - Handeni (km 65)

Kazi zilianza tarehe 15 Februari, 2010 zinatarajiwa kukamilika tarehe 14 Mei, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 63.2

xxiii. Barabara ya Chalinze-Segera - Tanga (km 245).

Mradi unagharamiwa na Serikali na DANIDA. Ukarabati umekamilika kwa sehemu ya Chalinze – Kitumbi (km 125), kwa sehemu ya Kitumbi-Tanga (km 120) kazi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2014.

xxiv. Barabara ya Korogwe (Segera) – Mkumbara – Same - Himo (km 254).

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika kwenye miaka ya 70 - 80. .Aidha, mchakato wa kumpata mkandarasi wa ukarabati kwa sehemu ya Korogwe – Mkumbara – Same (km 172) uko kwenye hatua za mwisho na unatarajiwa kuwa umekamilika ifikapo mwezi Novemba 2011. Ukarabati utagharamiwa kwa fedha za mkopo toka Benki ya Dunia.

xxv. Barabara ya Himo – Moshi – Arusha – Namanga (km 216)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwanzoni mwa miaka ya 90. Aidha ukarabati kwa sehemu ya Barabara ya Arusha - Namanga (km 105), kazi zilianza tarehe 14 Julai, 2008 na zinatarajiwa kukamilika Desemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 81.77 kwa fedha za Serikali na ADB/JICA.

xxvi. Barabara ya Himo – Horiri (km 11)

xxvii. Barabara ya Makuyuni – Ngorongoro (km 77)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2005 kwa fedha za msaada toka Serikali ya Japan

xxviii. Barabara ya Kilwa/Dar es Salaam (km 12).

Mkataba wa kumalizia kilometa 1.5 zilizobaki ulisainiwa tarehe 19 Oktoba 2010 na kazi ya ujenzi inatarajiwa kukamilika mwaka 2012.

xxix. Barabara ya Kawawa Junction - Mwenge-Tegeta (km 17).

kazi za ujenzi kwa sehemu ya Mwenge – Tegeta zinaendelea kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan. Aidha, sehemu ya Mwenge – Kawawa Junction (km 4.3) itafadhiliwa pia na Serikali ya Japan.

xxx. Barabara ya Dodoma - Iringa (km 260).

Ujenzi unagharamiwa na fedha za mkopo toka ADB na JICA na kazi zimegawanywa katika sehemu tatu. Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 13 Januari 2011 na kazi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2014.

xxxi. Barabara ya Uvinza - Kidahwe (km 76.6).

Kazi zilianza tarehe 24 Septemba 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 23 Juni 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 78.24 zikiwa ni kutoka Serikalini na mkopo kutoka Mfuko wa Abu Dhabi.

xxxii. Daraja la Malagarasi na barabara zake (km 48)

Mkataba ulisainiwa mwezi Oktoba 2010 na kazi inategemewa kukamilika mwaka 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 78.91 zikiwa ni kutoka Serikalini na mkopo Serikali ya Korea.

xxxiii. Barabara ya Mtwara – Mingoyo - Masasi (km 2005)
Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1977.

xxxiv. Barabara ya Dar es Salaam – Kibiti – Ikwiriri (km 165)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 1994 kwa sehemu ya Kibiti – Ikwiriri na sehemu ya Dar es Salaam – Kibiti mwaka 2008 kwa fedha za Serikali na OPEC.

xxxv. Masasi – Mangaka (km 55)

Ujenzi ulianza mwaka 2007 na umekuwa ukifanyika kwa awamu. Kazi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012 kwa gharama ya shilingi bilioni 30.184 kwa kugharamiwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la JICA.

xxxvi. Barabara ya Tunduru - Namtumbo (km 194).

Ujenzi unagharamiwa na fedha za mkopo toka Ujenzi unagharamiwa na fedha za mkopo toka ADB na JICA na kazi zimegawanywa katika sehemu tatu. Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 24 Desemba 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika mwezi Aprili 2013.

xxxvii. Barabara ya Namtumbo - Songea (km 70).

Ujenzi unaendelea kwa fedha za MCC na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 62.88.

xxxviii. Barabara ya Peramiho - Mbinga (km 78)

Ujenzi unaendelea kwa fedha za MCC na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 79.81.

xxxix. Barabara ya Tunduma - Sumbawanga (km 231)

xl. Barabara ya Mwanza – Nyanguge – Musoma – Sirari (km 305.9)

Ujenzi ulikamilika kwenye miaka ya 70 na ukarabati wa sehemu ya Mwanza – Nyanguge (km 35) ulifanyika mwaka 2000/2002 kwa fedha za EU

xli. Miradi ya Usanifu

Miradi ya usanifu iliyokamilika katika kipindi cha 2005/2010 ni;

Rujewa - Madibira-Mafinga (km 152), Mayamaya - Bonga (km 198.2), Nata - Fort Ikoma (km 141), Chaya - Nyahua (km 90), Mangaka - Mtambaswala (km 65), Mto wa Mbu – Loliondo – Mugumu - Nata-Makutano (km 452), Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Kamwanga - Sanya Juu (km 75), Uyovu – Bwanga - Biharamulo (km 112), Kisesa – Usagara (km 17), Sanya Juu - Bomang'ombe (km 25) na Katumba – Mbambo - Tukuyu (km 80).

Miradi ya usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami inayoendelea ni;

Bunda – Kisorya - Nansio (km 93), Ipole – Koga - Mpanda (km 255), Makurunge – Saadani – Pangani - Tanga (km 178), Matai - Kasesya (km 65), Same - Himo (km 96), Makambako – Songea (km 295), Mtwara – Masasi (km 200), Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 140), Tabora – Mambali – Bukene – Itobo - Kahama (km 149), Lupilo – Malinyi - Kilosa kwa Mpepo – Londo - Kitanda (km 396), Ifakara - Mahenge (km 67), Kibondo - Mabamba (km 35), Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi –Matala - Oldean Junction (km 328), Omugakorongo – Kigarama - Murongo (km 105), Mpemba - Isongole (Tanzania/Malawi) (km 49), Soni – Bumbuli – Dindira - Korogwe (km 74), Makofia – Mlandizi - Vikumburu (km 148), Kibaoni – Majimoto - Inyonga (km 162), Mpanda – Ugala – Kaliua – Ulyankulu - Kahama (km 428), Makongolosi – Rungwa - Mkiwa (km 412), Mtwara – Newala - Masasi (km 209), Handeni – Kiberashi – Kondoa - Singida (km 460), Kibaha - Mapinga (km 23), Geita – Bukoli - Kahama (km 107) na Mbande - Kongwa Junction - Mpwapwa (km 50).

### 7.1.6. *Miradi Mikubwa ya Madaraja*

i. Madaraja yaliyo kamilika kujengwa katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru

Kuna jumla ya madaraja 4,880 yaliyokamilika katika Barabara Kuu na Mikoa hadi kufikia 2011 nchi nzima. Baadhi ya madaraja makubwa yaliyokamilika ni;

Daraja la Kirumi lilikamilika na kufunguliwa na Rais wa Awamu ya Kwanza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tarehe 14 Oktoba, 1985. Daraja la Mto Kagera (1992), Daraja Rusumo (1974), Daraja la Mto Wami (1959), Daraja la Mto Ruvu (2008), Daraja la Mkapa (2003), Daraja la Umoja (2008), madaraja 11 katika barabara ya TANZAM, madaraja 7 katika barabara ya Tanga – Horohoro na Madaraja 4 katika barabara ya Tunduma - Sumbawanga.

ii. Madaraja yaliyo katika hatua za Usanifu na Ujenzi

a. Daraja la Kilombero

Usanifu wa Daraja la Mto Kilombero umekamilika na ujenzi utaanza mwaka 2011/2012.

b. Daraja la Mto Mwatisi

Kazi ya ujenzi wa Daraja la Mto Mwatisi inaendelea na kiasi cha shilingi milioni 870.0 kimekwisha tolewa. Gharama kulingana na mkataba wa kazi ni shilingi bilioni 1.39.

c. Daraja la Malagarasi

Ujenzi wa Daraja la Malagarasi umeanza kwa ufadhili wa Serikali ya Korea.

d. Daraja la Kigamboni

Serikali na NSSF wanaendelea na maandalizi ili kuanza ujenzi wa Daraja kwa njia ya *Public Private Partnership* katika mwaka wa fedha 2011/12.

### 7.1.7. *Miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam.*

Ili kukabiliana na tatizo la kupunguza msongamano wa magari Dar es Salaam hatua mbali mbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na;

i. Kujenga barabara ya Juu (Fly Overs) kwenye Makutano ya Barabara Maeneo ya TAZARA. Usanifu wa 'Flyover' ya TAZARA umeanza Juni 2011 kwa ufadhili wa JICA.

ii. Kupanua Mtandao wa Barabara za Jiji la Dar es Salaam kwa Kujenga na Kukarabati Barabara Zifuatazo:

iii. Barabara za Ubungo Bus Terminal – Mabibo - Kigogo Roundabout (km 6.4), Kigogo Roundabout - Bonde la Msimbazi –Twiga/Msimbazi Junction (km 2.7) na Jet Corner-Vituka-Davis Corner (km 10.3) kazi za ujenzi zinaendelea na zinategemewa kukamilika mwaka 2012.

iv. Aidha barabara za Tabata Dampo – Kigogo - Ubungo Maziwa External (km 2.25), Mbezi (Morogoro road) – Maramba Mawili – Kinyerezi - Banana (km 14), Tegeta - Kibaoni-Wazo – Goba - Mbezi Mwisho (km 20) na Tangi Bovu-Goba (km 9) usanifu umekamilika.

v. Barabara za; Old Bagamoyo - Garden Road (km 9.1), Kimara Baruti-Msewe-Changanyikeni (km 2.6) na Kimara – Kilungule - External Mandela Road (km 9) kazi za usanifu zinaendelea na zitakamilika mwaka 2012.

### *7.1.8. Mradi wa mabasi yaendayo kasi (DART) (km 20.9):*

Mradi wa mabasi yaendayo kasi (DART) una sehemu zifuatazo: -

i. Ujenzi wa barabara ya Kimara - Magomeni (km 10.4) na Magomeni – Kivukoni, Kawawa na Msimbazi (km 10.5):

ii. Mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea na mradi unafadhiliwa na Benki ya Dunia.

### *7.1.9. Wakala wa Barabara Nchini*

Moja ya mafanikio makubwa katika Sekta ya Barabara ni uanzishwaji wa Wakala wa Barabara Nchini (Tanzania National Roads Agency – TANROADS).

Wakala huu wa Barabara ulianzishwa chini ya Sheria Na 30 ya Mwaka 1997 (Executive Agencies Act No. 30/1997) na ulianza kazi mwezi wa Julai 2000. Wakala unahusika na Matengenezo, Ukarabati na Ujenzi wa Barabara Kuu na za Mikoa katika Tanzania Bara.

i. Dira ya Wakala

Katika utendaji wa kazi zake Wakala umejiwekea Dira, Mikakati na Sera ambazo zinaiongoza katika utekelezaji wa majukumu yake. Dira ya Wakala ni Kuwa na mtandao wa Barabara Kuu na Mikoa ambazo ni salama, endelevu, unaozingatia utunzaji wa mazingira na unaopitika majira yote ya mwaka, katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Tanzania.

ii. Dhamira ya Wakala

Kuendeleza, kufanyia matengenezo na kusimamia Barabara Kuu na za Mkoa kwa ufanisi zaidi kwa lengo la kuwa na mtandao wa barabara ulio endelevu na salama ambao unazingatia mkakati wa kupunguza Umaskini na Sera nyingine za Serikali.

iii. Majukumu ya Wakala

Majukumu ya Wakala ni kuratibu na kusimamia matengenezo, ukarabati na ujenzi wa Barabara kwenye mtandao wenye jumla ya kilometa 33,891 unaohusisha barabara Kuu (km 12,786) na barabara za Mikoa (km 21,105). Wakala unajihusisha pia na usimamizi wa Karakana za Mitambo ya Barabara pamoja na Kitengo cha Maabara Kuu ya Vifaa na Maabara za Mikoa. Aidha, Wakala husimamia pia jukumu la udhibiti wa uzito wa magari.

Wakala hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mikataba maalum na Mfuko wa Barabara kwa kazi za matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi kwa kazi za miradi ya maendeleo. Mafanikio yaliyokwishapatikana tangu kuanzishwa kwa Wakala hadi mwaka huu wa 2011 ni pamoja na;

Barabara zenye hali nzuri zimeongezeka kutoka asilimia 19 hadi 53:
Barabara zenye hali ya wastani zimeongezeka kutoka asilimia 32 hadi 36
Barabara zenye hali mbaya zimepungua kutoka asilimia 49 hadi 12


Daraja la Ruvu


Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akifungua rasmi barabara ya kutoka Usagara hadi Geita mnamo mwezi Mei 2011


Sehemu ya Barabara Kuu ya Kati

iv. Udhibiti wa Uzito wa Magari

Wakala umepewa jukumu la kudhibiti uharibifu wa barabara kutokana na magari kuzidisha uzito kupita viwango vilivyo ruhusiwa kisheria. Kwa kutekeleza hilo Wakala una mizani 22 ya isiyohamishika na 23 inayohamishika.

Jumla ya magari yapatayo 13,994,104 yalipimwa katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2010 na kati ya hayo 1,979,512 yalikuwa yamezidisha uzito na kutozwa faini. Fedha zilizopatikana kutokana na faini za kuzidisha uzito ni Shilingi bilioni 24.

Kutokana na mafanikio haya, kati ya Juni 30, 2001 na Juni 30, 2010 mtandao wa Barabara za lami kwa barabara Kuu na za Mkoa uliongezeka kutoka kilometa 3,972 mwaka 2000 hadi kilometa 6,500 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la kilometa 2,528 ndani ya Miaka 10. Kuimarika kwa mtandao wa barabara kumepelekea kupungua muda wa kusafiri barabarani mfano wakazi wa kanda ya ziwa walikuwa wanatumia zaidi ya saa 30 kusafiri kwa basi kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na hata wakati mwingine kulazimika kupitia nchi jirani kama vile Kenya (Nairobi). Kwa sasa (2011) wasafiri wanatumia muda wa chini ya saa 15 kwa safari hiyo. Aidha, kuboreka kwa mtandao wa barabara kumepelekea kupungua kwa gharama za usafirishaji.

Miradi iliyotekelezwa kwa kipindi hicho, miradi inayoendelea na iliyo katika hatua mbalimbali ya utekelezaji imefafanuliwa katika Sura 7 Aya ya 7.1.

v. Mikakati

a. Wakala kwa kushirikiana na wadau mbalimbali utaendelea kuwaelimisha wasafirishaji kuhusu umuhimu wa kutozidisha viwango vya uzito unaokubalika kisheria ili barabara zetu zidumu.

b. Wakala kwa kushirikiana na taasisi nyingine utaendelea kubuni namna ya kukuza uwezo wa makandarasi na wahandisi washauri wa ndani kwa lengo la kuongeza mitaji, ujuzi na uzoefu ili waweze kushindana kimataifa.

c. Jitihada zitaendelezwa kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wa barabara ili kudhibiti uharibifu wa vifaa mbalimbali kama alama za barabarani, madaraja, barabara zenyewe pamoja uhifadhi wa miliki ya barabara.

### 7.1.10. *Mfuko wa Barabara*

Bodi ya Mfuko wa Barabara ni moja ya mafanikio yaliyofikiwa katika sekta ndogo ya barabara na ilianzishwa mwaka 2000 ikiwa ni moja ya mikakati ya kuboresha Sekta ya barabara hususani katika kukusanya, kutoa na kuratibu matumizi ya fedha za matengenezo ya barabara. Serikali ilitunga Sheria ya ushuru wa Barabara (Marekebisho Na.2) ya 1998, iliyounda Bodi ya Mfuko wa Barabara na Mfuko wa Barabara. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2006, na kuitwa "Road and Fuel Tolls Act Cap 220, Revised edition 2006".

i. Vyanzo Vya Mapato


Hadi sasa vyanzo vya mapato kwa mujibu wa sheria ni kama ifuatavyo:

a. Ushuru wa barabara unaotozwa katika mafuta ya petroli na dizeli
b. Ushuru wa magari ya kigeni mipakani
c. Tozo ya magari yaliyozidisha uzito (hiki hakichukuliwi kama chanzo halisi cha mapato).

ii. Mafanikio ya Mfuko wa Barabara

Mfuko umekuwa kwa asilimia 741.8 kutoka shilingi billioni 40.03 mwaka 2000/2001 ulipoanzishwa hadi Shilingi billioni 296.95 mwaka 2010/2011.

**Chati inayoonyesha makusanyo ya Fedha za Mfuko wa Barabara kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi 2011.**



iii. Mikakati na Malengo ya Bodi kwa Miaka Ijayo.

a. Kuongeza ukubwa wa mfuko kwa kupanua wigo wa mapato ili kuweza kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara,

b. Kuongeza juhudi katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato,

c. Kuongeza uwezo wa kutumia fedha za mfuko hasa kwenye Halmashauri za Wilaya, na

## 7.2. UFUNDI NA UMEME

Katika kipindi cha miaka hamsini (50) ya Uhuru Serikali iliimarisha huduma za ufundi na umeme kama ilivyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

i. Magari ya Serikali na Mitambo

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, Wizara ya Ujenzi imekuwa ikishughulikia uandaaji wa ainisho la viwango na vipimo (specifications) na utunzaji wa kumbukumbu za magari ya Serikali kwa kuzingatia umuhimu wake katika kufanikisha utendaji na usafirishaji kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa nchi.

Baada ya Uhuru, Serikali imeendelea kuboresha na kujenga Karakana za Serikali kutoka Karakana nane (8) wakati wa upatikanaji wa Uhuru hadi kufikia karakana 21 ambazo zipo katika mikoa yote ya Tanzania bara zikitoa huduma ya matengenezo ya magari ya Serikali. Aidha, Mafundi na Wahandisi wa karakana hizi hususani Karakana Kuu ya M. T. Depot zilifanya kazi kubwa sana wakati wa vita kati ya nchi yetu na Uganda mwaka 1978 hadi 1979.

Wizara ya Ujenzi ilifanikisha kuandaa usajili wa magari yapatayo 21,000 ya Serikali ambayo yalikuwa yamesajiliwa kwa namba za kiraia na yalikuwa hayatambuliki kirahisi kuwa ni mali ya Serikali. Aidha, Wizara ilibuni namba za ST (magari ya Serikali Kuu), PT (magari ya jeshi la Polisi) na DFP (magari ya miradi iliyochini ya Wafadhili) kwa lengo la kusajili magari husika kulingana na majukumu yao na hivyo kuokoa fedha nyingi za Serikali.

Tangu kuanzishwa kwa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) idadi ya magari yaliyopatiwa matengenezo kwa nchi nzima ni 21,395. Aidha hadi sasa (2011) magari 65,252 ya Serikali yamesajiliwa.

ii. Vivuko vya Serikali vilivyopo (2011)

Wakati nchi inapata Uhuru wake mwaka 1961, hapakuwepo na vivuko vya kisasa, isipokuwa vivuko vitano (5) vya kuvutwa na kamba. Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa vivuko kama viungo muhimu kwenye barabara, iliendelea kununua na kujenga vivuko vya kutumia injini vinavyofikia 23 katika maeneo mengi ya nchi kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | MV. Ukombozi | Dar es Salaam | 1967 40t |
| b. | MV. Mwanza | Mwanza | 1968 40t |
| c. | MV. Geita | Mwanza | 1968 65t |
| d. | MV Utete I | Pwani | 1972 50t |
| e. | MV. Sabasaba | Ukerewe | 1972 85t |
| f. | MV. Pangani I | Tanga | 1973 35t |
| g. | MV. Chato | Mwanza | 1977 75t |
| h. | MV. Kome I | Mwanza | 1971 35t |
| i. | MV. Kilombero | Morogoro | 1985 40t |
| j. | MV. Sengerema | Mwanza | 1985 170t |
| k. | MV. Usiwe Kupe | Dar es Salaam | 1990 40t |
| l. | MV. Kigamboni | Dar es Salaam | 1990 170t. |
| m. | MV. Alina | Dar es Salaam | 1991 100t |
| n. | MV. Kilombero I | Morogoro | 2003 50t |
| o. | MV Nyerere | Mwanza | 2004 25t |
| p. | MV. Ilagala | Kigoma | 2005 50t. |
| q. | MV. Kilombero II | Morogoro | 2007 50t. |
| r. | MV. Ruhuhu | Ruvuma | 2008 50t. |
| s. | MV. Misungwi | Mwanza | 2008 250t. |
| t. | MV Magogoni | Dar es Salaam | 2008 500t. |
| u. | MV. Kome II | Mwanza | 2009 40t. |
| v. | MV. Pangani II | Tanga | 2010 50t. |
| w. | MV. Utete II | Pwani | 2010 50t |
| x. | MV Kilambo | Mtwara | 2004 50t |
| y. | MV Ruhuhu 1 | Ruvuma | 1997 7ton |
| z. | MV Rufiji | Pwani | 1985 40t |
| aa. | Kyanyabasa | Kagera | 2005 7 ton |

iii. Ununuzi wa Vivuko vipya kuanzia mwaka 2011

Aidha, hadi Septemba, 2011 ununuzi wa vivuko vifuatavyo ulikuwa katika hatua mabalimbali za utekelezaji;

a. Kivuko cha Mwigobero – Kinesi (Musoma), chenye uwezo wa kubeba tani 85.
b. Kivuko cha Kisorya (Bunda) – Rugezi (Ukerewe), chenye uwezo wa kubeba tani 85.
c. Kivuko cha Kilambo (Mto Ruvuma Mkoani Mtwara), chenye uwezo wa kubeba tani 50.

d. Kivuko cha Mtwara – Msanga Mkuu, chenye uwezo wa kubeba tani 50.
e. Kivuko cha Mto Ruvuvu (Rusumo Mkoani Kagera), chenye uwezo wa kubeba tani 35.
f. Kivuko cha Mto Malagarasi (Ilagala Kigoma), na
g. Kivuko cha Itungi Port (Kyela Mbeya)






Pamoja na ununuzi wa vivuko vipya, katika mwaka 2009 Serikali imevifanyia ukarabati mkubwa vivuko vyake vya MV Kigamboni (Dar es Salaam) na MV Sengerema (Mwanza). Serikali inakamilisha taratibu za kuvifanyia ukarabati mkubwa vivuko vya MV. Alina (Dar es Salaam) na MV. Pangani I (Tanga) katika mwaka wa fedha 2011/2012



Kivuko cha MV Magogoni kinacho toa huduma kati ya Magogoni na Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Kivuko hiki kina uwezo wa kubeba tani 500, sawa na abiria 2,000 na Magari 60



Kivuko cha zamani cha Ilagala mkoani Kigoma kilichokuwa kuvutwa kwa kamba



Kivuko kinachotumika (2011) Ilagala mkoani Kigoma kinachojiendesha chenyewe

iv. Ufungaji na Matengenezo ya Umeme Kwenye Majengo ya Serikali na Mashirika yake.

Mara baada ya Uhuru, Wizara ya ujenzi kupitia Idara ya Ufundi na Umeme ilikuwa ikifanya usanifu, kusimika mifumo ya umeme na kufanya matengenezo ya umeme katika majengo ya Serikali na Taasisi zake. Pamoja na shughuli hizi Idara ilikuwa inatengeneza mitambo na vifaa vya umeme kama; Jenereta, Viyoyozi, Majokofu, Mota, Vifaa vya Hospitali na elektroniki.

Katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa kazi za umeme, mitambo na vifaa vya umeme katika Serikali, Wizara katika miaka ya 1980 ilianzisha kikosi cha ujenzi kazi za umeme "Electrical Cooperation Sole". Hii ilichangia sana katika kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.

### *7.2.1. Wakala wa Ufundi na Umeme*

Kufuatia kukua na kuongezeka kwa kazi za ufundi na umeme ikiwa ni pamoja na mahitaji na sera ya Serikali kujitoa katika utendaji wa moja kwa moja, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya mwaka 1997 kwa tangazo la gazeti la Serikali Na. 254 la tarehe 26, Agosti, 2005. Hata hivyo Wakala ulizinduliwa rasmi na Serikali tarehe 23 Juni, 2006 na kuanza kutekeleza majukumu ya iliyokuwa Idara ya Ufundi na Umeme katika Wizara ya Ujenzi.

i. Majukumu ya Wakala

Majukumu ya Wakala huu ni kutoa huduma za Kihandisi kwa Serikali, Taasisi za Umma na watu binafsi katika nyanja za uhandisi wa mitambo, umeme na elektroniki. Majukumu haya yamegawanywa katika Idara zifuatazo:



ii. Uzalishaji na Matengenezo

Idara hii inashughulikia:

a. Matengenezo ya Magari na Mitambo ya Serikali katika Karakana ambazo zipo kila Mkoa,

b. Matengenezo na Usimikaji wa Mifumo ya Umeme, Mabarafu na Elektroniki, na

c. Matengenezo ya taa za kuongozea magari (Traffic lights) na taa za barabarani (Street Lights).



Mafundi wakiwa katika matengenezo ya magari katika moja ya karakana za TEMESA



Baadhi ya magari ambayo hukodishwa kwa ajili ya shughuli mbali mbali za Serikali

iii. Ukodishaji Mitambo na Huduma za Vivuko

Idara hii inashughulikia:

a. Ukodishaji wa Magari kwa ajili ya usafiri wa Viongozi (VIP Vehicles) yaliyopo katika Kitengo cha GTA (Government Transport Agency),

b. Ukodishaji wa Mitambo ya kuzalisha kokoto, na mitambo ya kazi za barabara iliyopo katika baadhi ya mikoa, na

c. Uendeshaji wa Vivuko vya Serikali katika Vituo 12 ambavyo ni Magogoni (Dar es Salaam), Kilombero (Morogoro), Pangani (Tanga), Ruhuhu (Ruvuma), Kilambo (Mtwara), Kigongo/Busisi (Mwanza), Rugezi/Kisorya (Mwanza/Mara), Bugolora/Ukara (Mwanza), Nyakaliro/Kome (Mwanza), Chato (Mwanza/Kagera), Kyanyabasa (Kagera), Ilagala (Kigoma) na Utete (Pwani).

iv. Ushauri wa Kiufundi.

Idara hii inashughulikia:

a. Ushauri wa Kiufundi kwa Serikali na Umma kwa ujumla katika nyanja za uhandisi wa Mitambo, Umeme na Elektroniki,

b. Ushauri wa kiufundi kuhusu usimikaji wa mifumo mipya ya uhandisi wa Mitambo, Umeme na Elektroniki, na

c. Usanifu na Usimamizi wa usimikaji wa mifumo ya uhandisi wa mitambo, umeme na elektroniki ili kukidhi viwango vinavyotakiwa na kwa kulingana na matakwa ya Sheria na Taratibu zinazoongoza taaluma husika.

v. Utekelezaji wa majukumu ya Wakala na Mafanikio

Mpango wa Maendeleo wa Wakala

Kuanzia Julai 2006 Wakala wa Ufundi na Umeme ulianza rasmi kutekeleza kazi zake kupitia Mpango wake wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2006/2007. Mpango huu ulizingatia Mpango – Mkakati wa Wakala wa miaka mitano (2005 – 2010) *(TEMESA Strategic Plan 2005 – 2010).*

Kwa sasa Wakala umeanza kutekeleza Mpango Mkakati wake wa pili wa miaka mitano wa kuanzia 2011/12 hadi 2015/16, ambao unaanza kutekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

vi. Mafanikio

Kuanzia mwaka 2006, Wakala umetekeleza kazi zake na kupata mafanikio yafuatayo:

a. Kufanya usanifu wa miradi 270, kusimamia miradi 299, kufanya mapitio ya michoro ya kihandisi 47, na kutoa ushauri katika miradi 374 ya kihandisi katika Idara za Serikali na Taasisi mbali mbali za Umma,

b. Wakala kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi –ERB kama Taasisi ya Ushauri (Consulting Firm) katika kazi za Uhandisi pamoja na kuwasajili Wahandisi wake 5 kwa ajili ya kazi hizo (Consulting Engineers). Hii imesaidia kuipatia TEMESA jina miongoni mwa Taasisi za Kihandisi nchini ikitiliwa maanani kwamba Wakala unao Wahandisi wengine zaidi ya 20 ambao wamesajiliwa kama Wahandisi Wataaluma "Professinal Engineers"; na pia Wakala umesajili vitengo vyake viwili (Mabarafu na Viyoyozi na Electroniki zote katika Daraja la II) na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB),

c. Kutokana na miongozo na uangalizi wa Wizara, Wakala umeendelea kusimamia uendeshaji wa vivuko vya Serikali. Hali hii imeuwezesha Wakala kuendelea kuboresha huduma za Vivuko kwa wananchi wanaotumia huduma hizo nchini,

d. TEMESA imeendelea kuboresha huduma za matengenezo ya magari na usimikaji wa mifumo ya umeme katika Karakana zake nchi nzima (Tanzania Bara). Wakala umeanza ukarabati mkubwa

wa karakana ya MT. Depot na ujenzi wa karakana mpya ya Mkoa wa Manyara,

e. Wakala umeendelea kutoa mafunzo kwa Viongozi wa karakana na mafundi ili kuimarisha utendaji kazi wao, na

f. Ununuzi wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kununua mitambo maalum ya kisasa ya kutambua matatizo ya magari (computerized diagnostic machines) kwenye karakana ya MT. Depot.

vii. Mikakati ya Miaka Ijayo

Ili kuweza kuongeza ufanisi na kufanikisha malengo ya kuanzishwa kwake, TEMESA inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

a. Kuboresha uwezo wa ukusanyaji mapato:

TEMESA inandaa mkakati wa kufuatilia na kukusanya mapato katika Vituo vyake vyote ambapo pamoja na mambo mengine, utawekwa utaratibu wa kuwa na mikataba ya kutekeleza kazi baina yake na wateja (Service Level Agreements – SLAs).

b. Kuweka mikakati endelevu ya huduma za Vivuko

Kuboresha miundombinu ya kuhudumia abiria ikiwa ni pamoja na kuweka Mashine za kisasa za kukatisha Tiketi (Automatic Vending and Validating Machines) katika Vivuko vyote nchini,

Kuingia ubia na sekta binafsi katika kuanzisha usafiri wa majini katika fukwe kati ya Magogoni na Bagamoyo ili kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es salaam.

Kuendelea kufanya tafiti zitakazowianisha mahitaji ya huduma ya vivuko na idadi ya vivuko.

Kutumia vivuko kama njia mojawapo ya kupunguza msongamano wa magari mijini hususan dar es Salaam, Mwanza, Tanga n.k.

c. Kuweka mikakati endelevu ya kuboresha Karakana

Wakala utaendelea kuboresha karakana zake kwa kuzifanyia ukarabati mkubwa na kununua vitendea kazi vya kisasa ili kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya wateja.

d. Mafunzo kwa Kada zote za watumishi

TEMESA itaendelea kuboresha mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wa Wakala ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Inatarajiwa kuwa mafunzo haya yatakuwa kichocheo cha kuongeza tija ndani na nje ya Wakala.

## 7.3. WAKALA WA MAJENGO

Wakala wa Majengo (Tanzania Buildings Agency – TBA) ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya 1997 kutokana na iliyokuwa Idara ya Majengo ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi. Ulizinduliwa rasmi tarehe 17 Mei 2002 kwa madhumuni ya kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa kutumia njia za kibiashara na uongozi bora wa fedha ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi. Majukumu ya wakala ni kama yafuatavyo;

i. Matengenezo ya Majengo ya Serikali

ii. Ujenzi wa nyumba mpya kwa ajili ya viongozi wa Serikali

iii. Kusimamia miradi ya ujenzi na kutoa huduma ya ushauri kwa Majengo ya Serikali

iv. Kutoa ushauri kwa Serikali kuhusiana na masuala yote yahusuyo nyumba

v. Ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Wakala

vi. Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kuwauzia watumishi wa umma

vii. Upangishaji wa nyumba za Serikali kwa watumishi wa umma

viii. Upangishaji wa baadhi ya nyumba za Serikali kibiashara.

### *7.3.1. Mafanikio ya Miaka Hamsini (50) ya Uhuru*

Katika kipindi cha miaka hamsini (50) ya Uhuru Serikali kupitia Wakala wa Majengo imejenga na kukarabati nyumba za viongozi na watumishi wa Serikali katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara pamoja na kuratibu shughuli za Wakala wa Majengo ili kujenga nyumba za watumishi kwa lengo la kupunguza uhaba wa nyumba za kuishi watumishi wa umma.

Katika kipindi hicho Serikali imejenga majengo ya ofisi kwa ajili ya matumizi ya baadhi ya Wizara, makao makuu ya mkoa wa Manyara, makao makuu ya wilaya mpya za Chato, Nkinga, Siha na Nanyumbu na nyumba mpya za kuishi watumishi katika mikoa yote zikiwemo nyumba za ghorofa kwa ajili ya makazi ya Waheshimiwa Majaji na Mawaziri.

Wakala wa Majengo umesimamia ujenzi wa nyumba 1,026 katika maeneo ya Boko, Mbweni na Ubungo (Dar es Salaam), Kisasa (Dodoma), Njiro (Arusha), Chato (Kagera), Mkinga (Tanga), Siha (Kilimanjaro) na Nayumbu (Mtwara) zenye thamani ya Tshs. 40,578,937,302.80 kati ya mwaka 2002/2003 hadi Juni 2011. Kati ya nyumba hizo Wakala umejenga nyumba 861 za thamani ya kiasi cha Tshs 24,943,924,573.00 kutoka katika vyanzo vya fedha zake na imesimamia ujenzi wa nyumba 165 za thamani ya kiasi cha Tshs 15,635,012,729.80 kwa fedha iliyotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi.

Aidha, Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa Ikulu, jengo la Mahakama ya Biashara Kivukoni na kuweka katika mipango yake taratibu za muda mfupi na mrefu za kukarabati majengo ya ki-historia ili kuhifadhi historia ya nchi kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Katika kutekeleza azma hii, Serikali inakarabati jengo la kihistoria Bagamoyo ambalo lilitumika kama Boma wakati wa utawala wa Wajerumani. Awamu ya kwanza ya ukarabati wa jengo hilo ilianza mwaka 2008/09 kwa kufanya upembuzi yakinifu na kukamilisha michoro. Awamu ya pili ya ukarabati wa jengo hilo inaendelea.






Nyumba za Viongozi na Watumishi wengine wa Serikali ambazo zimekuwepo tangu wakati wa Uhuru wa Tanzania Bara





**Nyumba kwa ajili ya Viongozi wa Serikali na Watumishi wa Umma zinazotumika kwa sasa (2011)**





### *7.3.2. Viwanja/Mashamba ya Wakala wa Majengo (TBA)*

i. Hadi kufikia Juni, 2011 Wakala ulikuwa na jumla ya viwanja 2,033 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na mashamba ambayo hayajagawanywa viwanja ambapo yakigawanywa jumla ya viwanja vyote inakuwa 4,608.

ii. Mashamba ambayo Wakala umenunua Dar es Salaam na Mikoani ni kama ifuatavyo;-

  a. Manispaa ya Temeke eneo lenye jumla ya viwanja – 200;
  b. Kibaha Pwani - Ekari 36.84;
  c. Tunduma – Ekari 774.3;
  d. Itega Dodoma – Ekari 5;
  e. Nzuguni Dodoma -Ekari 630; na
  f. Kiluvya- Pwani -Ekari 1000.

Viwanja vya Nzuguni-Dodoma, Bunju na Kiluvya–DSM vinatarajiwa kuendelezwa kwa njia ya PPP (Public, Private Partnership).

### *7.3.3. Malengo na Mwelekeo kwa Wakati Ujao*

i. Wakala unakusudia kuanza kutekeleza mpango wa ujenzi wa nyumba elfu kumi (10,000) za watumishi wa umma nchi nzima kuanzia mwaka huu 2011. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka mitano ijayo;

ii. Kuendelea kushirikiana na Wizara, Wakala zingine na Taasisi za Serikali;

iii. Kuboresha zaidi utoaji wa huduma ya ushauri kwa Serikali na taasisi zake.

## 7.4. USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA

Mnamo mwaka 1992 Wizara ya Ujenzi iliunda Kitengo cha Usalama Barabarani (Road Safety Unit) ambacho kilikuwa chini ya Idara ya barabara. Kitengo hicho kiliundwa kwa madhumuni ya kushughulikia masuala mbalimbali yanayohusu usalama barabarani.

Kutokana na kuongezeka kwa shughuli za usalama na umuhimu wa mazingira katika Miundombinu ya Usafirishaji, mwaka 2008 Wizara ya Ujenzi (wakati Wizara ya Miundombinu) iliunda Idara ya Usalama na Mazingira kwa madhumuni ya kushughulikia masuala yote ya Usalama na Mazingira katika miundombinu ya usafirishaji.

### *7.4.1. Mafanikio katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru*

Kuanzia mwaka 1992 chini ya kitengo cha usalama barabarani majukumu yafuatayo yalitekelezwa;

i. Kuandaa 'Road Safety Progromme' mwaka 1995

ii. Kuandaa kanuni ya usimamizi wa mizigo (Maximum weight of vehicles regulation) ya mwaka 2001 ambayo ilitokana na sheria ya mwaka 1973 kifungu cha 114 (2P)

iii. Kutengeneza 'National Road Safety Master Plan' Tanzania Bara na Zanzibar ambayo ilikamilika mwaka 2004

iv. Kufanya utafiti wa ajali za barabarani Tanzania bara mwaka 2007

v. Kusimamia udhibiti wa uzito barabarani kuanzia mwaka 1992

vi. Kutoa elimu ya usalama barabarani kwa wadau wa barabara kupitia magazeti, radio, vipeperushi, televisheni na mabango ya matangazo (billboards).

vii. Kutoa elimu ya usalama barabarani mashuleni

Kuanzia mwaka 2008 chini ya idara ya Usalama na Mazingira yafuatayo yalitekelezwa;

### *7.4.2. Menejimenti ya Usalama*

i. Kuandaa Sera ya Kitaifa ya Usalama Barabarani yenye malengo yafuatayo:-

   a. Kuhakikisha barabara zetu haziharibiwi na uzito wa gari au uzito kwenye (axle) au zote kwa pamoja wakati wa usafirishaji.

   b. Kulinda usalama wa watumiaji wa barabara na uwekezaji kwenye shughuli za usafirishaji

   c. Kuhakikisha usanifu (design) wa barabara zetu na madaraja ni salama kwa faida ya watumiaji na uwekezaji

d. Kuwa na magari ya viwango vinavyokubalika ili kudhibiti usalama wa magari kutumia barabara zetu

e. Kuanzisha vituo vya kujaribia madereva na utoaji leseni ili kuwa na madereva makini katika barabara zetu.

f. Kupunguza tatizo la uegeshaji mbaya wa magari ili kuongeza uwezo na usalama wa barabara zetu.

g. Watoto kuweza kupata elimu sahihi ya matumizi ya barabara, na kusaidia kupunguza namba ya vifo na majeruhi kwa watoto na kupata watumiaji bora wa barabara siku zijazo.

h. Kujenga nidhamu kwa watumiaji wa barabara kwa kuwapatia elimu ya sheria ya usalama barabarani, kanuni na athari za ajali.

i. Kuonyesha matatizo ya usalama barabarani yanayosababishwa na matumizi ya mipango miji.

j. Kuanzisha na kuendeleza mfumo sahihi wa ukusanyaji rekodi za ajali zote za barabarani na kutumiwa na wadau wote wa usalama barabarani kwa;

    Kutengeneza vitabu vya kanuni za barabara na mwongozo wa madereva wanafunzi ambao una mtaala kwa ajili ya shule za udereva

    Kutengeneza kitabu cha mwongozo wa uwekaji alama za barabarani

    Kutengeneza kitabu cha mwongozo wa ukaguzi wa Usalama wa Barabara (Road Safety Audit)

### *7.4.3. Menejimenti ya Mazingira*

Wizara ya Ujenzi kupitia ufadhili wa DANIDA na mfuko wa Barabara imeshaandaa vitendea kazi kwa ajili ya Usimazi na Uhifadhi wa Mazingira vifuatavyo:

i. Mkakati Endelevu wa Kuboresha Mazingira ya Barabara (Sustainable Development Strategy),2004

ii. Mwongozo wa kutathmini na kuhifadhi mazingira ya barabara (Environmental Assessment and Management Guidelines 2004 EA&MG), 2009.

iii. Compensation and Resettlement Guidelines for the Road Sector, 2009

iv. Strategic Environmental Assessment Guidelines for the Roads Planned for Construction in Tanga Region 2007/2008

v. Environmental Information Management System for Road Sector, 2010

vi. Kanuni za kuzuia uharibifu wa mazingira ya barabara (Road Sector Environmental Protection Regulations,2010)

Mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Usimamizi wa Mazingira ya Barabara kwa Kwa Wahandisi, Mafundi Sanifu, Wataalamu Washauri na Makandarasi yalifanyika. Lengo lilikuwa ni kutoa elimu ya weledi wa mazingira katika utekelezaji wa miradi ya barabara kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kitaifa na ya kimataifa iliyoyopo. Aidha Wahandisi 300, mafundi sanifu 352, Wataalamu Washauri 15 na makandarasi 10 walipata mafunzo haya.

Miradi ya barabara zaidi ya 30 ilifanyiwa tathmini ya Athari kwa Mazingira kabla ya utekelezaji wake

### *7.4.4. Mipango ya Miaka ijayo*

Menejimenti ya Usalama

i. Kuanzisha Wakala wa Taifa wa Usalama Barabarani

   a. Kuanzisha 'Drivers and Vehicle Examination Licensing Agency' (DVELA)

   b. Kujenga na kusimamia sehemu za kupumzikia madereva na abiria katika Barabara Kuu "Compulsory Resting Stations and Refreshment Areas"

   c. Kuwa na mizani ambayo ni 'Automatic recording and Weigh in Motion'

   d. Kuboresha mizani kutoka kwenye "Group Axle Weighing" kwenda kwenye 'Single Axle Weighing'.

ii. Menejimenti ya Mazingira

   a. Kuandaa Mpango Kazi wa Miaka Mitano wa Mazingira kwa ajali ya Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, na vitendea kazi tajwa hapo juu

b. Kujenga vituo vya kupunzika ambavyo vitakuwa na vyoo kaatika barabara zote kuu ili kupunguza utupaji taka holela unaosababisha kuziba kwa mitaro ya maji mvua

c. Kuhakikisha kuwa mashimo yote yanayotoa mali ghafi za ujenzi yanafunikwa kitaalumu na kupanda miti kwa ajili ya kulinda ecolojia na kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

## 7.5. SERA NA SHERIA

Katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru, Wizara imeandaa Sera na Sheria mbali mbali kama ifuatavyo;

i. Sheria ya barabara ya mwaka 1932 iliyokuwa inatumika mara baada ya Uhuru ('Highways Ordinance Cap) ilifanyiwa marekebisho mwaka 1967. Kwa kuzingatia mabadiliko na mahitaji, sheria ya barabara, Sheria namba 13 ilitungwa mwaka 2007.

ii. Sera ya Taifa ya Usafiri na Usafirishaji nchini ya mwaka 2003 "National Transport Sector Policy, 2003" ambayo pamoja na mambo mengine inasisitiza:

iii. Sera ya Taifa ya Ujenzi ya mwaka 2003 (Construction Industry Policy, 2003) ambayo pamoja na mengine inasisitiza yafuatayo.

iv. Sera ya Usalama Barabarani ya mwaka 2010 (Road safety policy 2010)

Matokeo ya kuwepo kwa Sera umepelekea kuanzishwa kwa Taasisi za: Baraza la Taifa la Ujenzi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Kikosi cha Ujenzi, Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia ya Nguvukazi nchini, Chuo cha Ujenzi cha Morogoro, Kitengo cha Ushirikishwaji wa Wanawake.

## 7.6. BARAZA LA TAIFA LA UJENZI (NCC)

Ili kuboresha na kuimarisha juhudi za kazi za ujenzi hapa nchini, Serikali mnamo mwaka 1979 kwa Sheria namba 20 ilianzisha Baraza la kusimamia maendeleo ya Sekta ya Ujenzi kwa ajili ya uratibu, ushauri, usimamizi na kukuza taaluma ya ufundi kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia na mwenendo wa ufanisi.

### *7.6.1. Mafanikio katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru.*

Baraza limeratibu na kufanikisha kuundwa kwa Sera ya Ujenzi mwaka 2003 na mpango wake wa utekelezaji; kuandaliwa kwa Mkakati wa maendeleo ya Sekta ya Ujenzi mwaka 1990; utayarishaji wa Rasimu na Mwongozo wa Sera ya ubia kati ya sekta ya umma na Binafsi mwaka 2008; uanzishwaji wa vyama mbalimbali vya ushauri na bodi za usajili; kuandaa makongamano ya Sekta ya Ujenzi kitaifa na kimataifa; kutoa huduma za ushauri na usuluhishi wa migogoro; uendeshaji wa Mafunzo na Tafiti; uandaaji wa machapisho ya kitaalamu; na Ukaguzi wa Miradi.

## 7.7. BODI YA USAJILI WA WAHANDISI

Kazi za ujenzi zinafanyika kwa taaluma kuzingatia ubora, uwezo na ufanisi wa Wahandisi ambao hawana budi kukidhi vigezo vya kitaaluma na ueledi. Kwa kuzingatia hitaji hili muhimu, Serikali kupitia sheria namba 49 ya mwaka 1968 pamoja na marekebisho yaliyofuata, chini ya Sheria Namba 15 ya Mwaka 1997 ilianzisha Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB) na Namba 24 ya 2007 yenye majukumu ya kuratibu na kusimamia mienendo na shughuli za kihandisi nchini.

Bodi imeweka vipengele 8 vya usajili wa Wahandisi kwa kuzingatia elimu na uzoefu wa mhusika, vikihusisha wenye Vyeti, Stashahada, Stashahada ya Juu, na Shahada za juu, pamoja na mafunzo kwa vitendo na uzoefu.

### *7.7.1. Mafanikio ya Bodi katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru*

Kumekuwa na mafanikio makubwa katika kuboresha uwepo wa wataalamu hawa ambapo usajili wao umekuwa ukiongezeka. Kwa mfano, mwaka 1961 Wahandisi wazalendo walikuwa 2 tu waliosajiliwa ambapo mwaka 2011 wamefikia 10,410.

## 7.8. BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI

Kwa kuzingatia sera ya kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kazi za ujenzi na huduma za ujenzi suala lilokuwa sambamba na kuongezeka kwa matumizi ya makandarasi, Serikali kupitia sheria namba 17 ya mwaka 1997 ilianzisha Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) ili kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za makandarasi katika soko huria. Bodi inayo dhamana ya kusajili Makandarasi, kuratibu shughuli na mwenendo wa makandarasi wote na kujenga uwezo wa makandarasi wa kitanzania.

### *7.8.1. Mafanikio ya Bodi kwa kipindi cha miaka 50 ya Uhuru*

Kwa mujibu wa kumbukumbu ambazo Bodi inazo, kabla ya kuanzishwa kwake 1997 kulikuwa na jumla ya makandarasi 900. Aidha toka kuanzishwa kwake, Bodi imeweza kusajili jumla ya makandarasi zaidi ya 7,000.

Tangu kuanzishwa kwa Bodi, jumla ya miradi 12,600 imekaguliwa. Aidha kwa kuzingatia usimamizi wa sheria jumla ya kesi 254 zimefikishwa mahakamani.

Bodi imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa makandarasi ili kuboresha uwezo wao. Mpaka kufikia Juni 2011 makandarasi 2,895 wamenufaika na mafunzo. Bodi imeanzisha taratibu za kuwasaidia makandarasi kujenga uwezo kwa kuwepo na mfuko unaotoa dhamana kwa ajili ya zabuni (Bid Bonds) na malipo ya awali (Advance Payment Gurantees). Hadi kufikia Juni 2011 mfuko una kiasi cha TZS 2.0 billioni na makandarasi 860 wameshajiunga na kunufaika na mpango huo.

## 7.9. BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI

Udhibiti wa taaluma ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi nchini ni jambo lililoanza kutambulika chini ya Sheria Namba 37 ya mwaka 1949 pamoja na sheria ndogondogo za mwaka 1950. Baada ya Uhuru, Wizara iliendelea kutambua na kusajili wanataaluma hawa ambapo kwa Sheria Namba 16 ya mwaka 1997, iliundwa Bodi iliyopewa jukumu la kuratibu shughuli za makampuni ya utoaji wa huduma katika fani hii husika na mwaka 2010 kuliongezeka jukumu la kuratibu kada za kati na fani ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi ili kukidhi mahitaji ya wakati katika sekta ya ujenzi kwa ujumla.

### *7.9.1. Mafanikio ya Bodi kwa kipindi cha miaka 50 ya Uhuru*

Bodi imesajili wanataluma 527 ikilinganishwa na wataalm 10 waliokuwa wamesajiliwa hadi mwaka 1974.

Kati ya Wataalam hao waliosajiliwa kati yao Wabunifu Majengo ni 328 na Wakadiriaji Majenzi ni 199, vilevile yamesajiliwa makampuni 171 ya Wabunfu Majengo na makampuni 72 ya Ukadiriaji Majenzi.

Bodi pia imejishughulisha na ukaguzi wa miradi mbali mbali kuhakiki ubora wa kazi na kuratibu kufuatwa kwa taratibu zilizowekwa na kutoa fursa za wahusika kupata mfunzo ya elimu endelevu na midahalo ya kitaaluma kuwafikia wadau husika.

## 7.10. KIKOSI CHA UJENZI

Kufuatia makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China, mnamo mwaka 1974 kilianzishwa Kikosi cha Ujenzi kwa sheria Namba 23. Kikosi hiki ndicho kilichorithi majukumu na wafanyakazi waliojenga reli ya TAZARA baada ya mradi huo kukamilika. Majukumu ya Kikosi hiki ni pamoja na; ujenzi na ukarabati wa majengo kwa niaba ya Idara ya ujenzi; ujenzi wa majengo mbalimbali ili kufanya biashara na kutoa

huduma. Kikosi kimesajiliwa na Bodi ya kusajili Makandarasi na makao yake makuu yako Dar es Salaam huku kikiwa na matawi katika mikoa ya Dodoma, Arusha na Mwanza.

### *7.10.1. Mafanikio ya Kikosi kwa kipindi cha miaka 50 ya Uhuru*

Kikosi kimeweza kutekeleza miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa majengo kwa ufanisi mbali na kukabiliwa na ushindani mkubwa wa soko huria na kuwa na uwezo mdogo wa mtaji.

Baadhi ya miradi iliyotekelezwa katika kipindi hicho ni kama ifuatayo:-

i. Ujenzi wa nyumba za kuishi watumishi wa umma – 5 Ubungo, Dar Es salaam,na 10 jijini Mwanza,

ii. Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi ya Waziri Mkuu – Dodoma,

iii. Ujenzi wa "Concrete Box Culverts "Kigogo/Tabata, Dar Es Salaam,

iv. Ujenzi wa "Community Centres' – Mafia, Kilwa na Rufiji,

v. Ujenzi wa Bweni la wanafunzi Chuo cha Wauguzi Lindi,

vi. Ujenzi wa kituo cha Hali ya Hewa Singida,

vii. Ujenzi wa uzio wa " Rest House" ya Serikali Dodoma,

viii. Ujenzi wa nyumba za viongozi Dar es Salaam na Mwanza,

ix. Ukarabati wa ofisi katika Bohari kuu ya Serikali Dar es Salaam,

x. Ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya Nyamagana, Mwanza,

xi. Ujenzi wa maegesho (ferry ramps) ya kivuko Kinesi Rorya, Mara,

xii. Ukarabati na uhifadhi wa Jengo la Old Boma Bagamoyo, Pwani,

xiii. Ukarabati wa Ofisi na Ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Korogwe, Tanga,

xiv. Utengenezaji na usimikaji wa malango ya kuingilia Ikulu na kwenye makazi ya Waziri Mkuu, Dar es Salaam,

xv. Ujenzi wa Uzio kwa ajili ya ofisi na karakana ya TEMESA Babati, Manyara,

xvi. Ujenzi wa uzio (Concrete Fence) Ikulu – Dar Es Salaam, na


xvii. Ujenzi na ukarabati wa majengo ya mitambo ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

## 7.11. CHUO CHA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA STAHILI YA NGUVUKAZI

Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia ya Nguvukazi nchini (ATTI), ni taasisi ya Serikali iliyopo chini ya Wizara ya Ujenzi. Chuo hiki kipo wilayani Rungwe, mkoa wa Mbeya. Tangu kuanzishwa kwake mnamo mwaka 1993, chuo kimeshaendesha mafunzo mbalimbali juu ya teknolojia ya nguvukazi (Labour Based Technology – LBT) katika kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini kwa wataalam mbalimbali wa sekta ya umma na binafsi.

### *7.11.1. Mafanikio ya Chuo*

Katika kipindi cha miaka 18 ya uhai wake, chuo kimefundisha jumla ya wahitimu wapatao 1,929 toka kada mbalimbali katika sekta ya umma na binafsi kama ilivyoonyeshwa katika Chati.




## 7.12. CHUO CHA UJENZI MOROGORO

Chuo cha Ujenzi Morogoro kilianzishwa mara tu baada ya Uhuru wa Tanganyika kupatikana mwaka 1961 huko Mgulani Dar es Salaam kama Chuo cha Ufundi Stadi (Trade School). Majukumu yake yalikuwa kutoa mafunzo kazini na kuwaendeleza watumishi wa Serikali. Chuo hicho kilikuwa chini ya Wizara ya Kazi, Maji, Ujenzi na Uchukuzi kwa wakati huo. Baadae mwaka 1972 Wizara hiyo iligawanywa. Chuo hicho kiliwekwa chini ya Wizara ya Kazi, Ujenzi na Uchukuzi. Mnamo mwaka wa 1974 Chuo hicho kilihamishiwa Morogoro na kuitwa Chuo cha Ujenzi Morogoro (Morogoro Works Training Institute – MWTI).





Wafanyakazi wakiwa mafunzoni

### *7.12.1. Mafanikio ya Chuo*

Katika kipindi cha miaka 49 tangu kuanzishwa kwa Chuo, Wafanyakazi wengi wa kada za chini na kati walipitia chuoni kupata mafunzo ya awali ya ujenzi au kujiendeleza. Mafunzo hayo yamekuwa chachu katika sekta ya ujenzi ya umma na binafsi.

## 7.13. KITENGO CHA USHIRIKISHWAJI WA WANAWAKE KATIKA KAZI ZA BARABARA

Wizara ilianzisha Kitengo cha Ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za barabara mnamo mwaka 1992/93. Kitengo hiki Kipo chini ya Idara ya barabara za Mikoa. Lengo kuu la kuanzishwa kitengo hiki ni kuwahamasisha wanawake kushiriki katika kazi za barabara ili kuwepo kwa uwiano sawa wa kijinsia na kujiongezea kipato hivyo kupunguza umaskini katika jamii.

Ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za ujenzi na matengenzo ya barabara kitaifa ulianza mwaka 1992, katika mikoa ya Mbeya, Tanga, Shinyanga, Mwanza na Mtwara.

Kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 1994 Serikali ya Tanzania iliendesha mradi wa ukarabati na matengenezo ya barabara katika mikoa ya Lindi na Mtwara chini ya Rural Integrated Support Programme (RIPS) kwa msaada wa Serikali ya Finland ambao ulihamasisha wanawake kushiriki katika kazi za barabara.



Akina mama katika mafunzo ya kazi za ujenzi

Mwaka 1998 Serikali za Tanzania na Finland zilianzisha mradi wa majaribio ulioshirikisha wanawake kufanya ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini katika mikoa ya Lindi na Mtwara na kufuatiwa na utekelezaji wa mradi awamu ya pili ya Matengenezo na Ukarabati wa Barabara za Mikoa ya Lindi na Mtwara ulioanza mwaka 2000 na kwisha mwaka 2002.

### *7.13.1. Mafanikio ya Kitengo kwa Kipindi cha miaka 50 ya Uhuru*

Kutokana na mradi hiyo, katika mikoa ya Mtwara na Lindi kuna idadi ya kuridhisha ya Ushiriki wa Wanawake katika kazi za barabara. Kwa mfano mradi wa kukarabati kilometa saba (7 km ) ya barabara ya Libobe – Kitere , uliodhaminiwa na ILO kama mradi tangulizi (Pilot Project) asilimia 66 ya wafanyakazi walikuwa wanawake.

Kitengo kimekuwa kikiwezesha kufanyika kwa mafunzo mbalimbali juu ya ushiriki wa wanawake, katika kazi za barabara kwa kutumia teknolojia ya Nguvu Kazi (Labour Based Technology – LBT) kwa vikundi vya wanawake na wanawake Makandarasi. Kitengo kimewezesha kufanyika kwa mafunzo ya muda mfupi kwa vikundi vya wanawake na wanawake makandarasi ya namna ya kujenga na kuzifanyia matengenezo barabara kwa kutumia teknolojia ya Nguvu Kazi katika mikoa ya Tanga na Morogoro katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 na 2010/2011.

Kuwahamasisha na kuwahimiza wanawake kuanzisha makampuni na vikundi vya kufanya kazi za ukandarasi . Mpaka kufikia mwezi Mei mwaka 2011 kuna idadi ya Makandarasi wanawake wa barabara 120 na 68 wa majengo

Kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara kila mwaka kutoka asilimia 7 wakati mpango ulipoanza hadi wastani wa asilimia 35. Matarajio ni kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2015.



Akina mama wakiwa katika kazi za barabara

## 8. HITIMISHO

**'Tumethubutu, Tumeweza Tunazidi Kusonga Mbele'**

**Barabara**
Mtandao wa barabara za lami umeongezeka kutoka kilometa 1,360 zilizokuwepo wakati tunapata Uhuru hadi kufikia kilometa 6,500 wakati sasa (2011). Aidha, zaidi ya kilometa 11,154 ziko katika hatua mbali mbali za ujenzi kwa kiwango cha lami.

Serikali imeweza kubuni Mradi Maalum wa kujenga barabara za lami kwa kutumia fedha za ndani na miradi zaidi ya 40 tayari inatekelezwa kwa kiwango cha lami.

'Tumethubutu, Tumeweza Tunazidi Kusonga Mbele'

**Nyumba**
Wakati tunapata Uhuru zilikuwepo nyumba 6,000.

Wakala wa Majengo umesimamia ujenzi wa nyumba 1,026 katika maeneo ya Boko, Mbweni na Ubungo (Dar es Salaam), Kisasa (Dodoma), Njiro (Arusha), Chato (Kagera), Mkinga (Tanga), Siha (Kilimanjaro) na Nanyumbu (Mtwara) zenye thamani ya Tshs. 40,578,937,302.80 kati ya mwaka 2002/2003 hadi Juni 2011. Kati ya nyumba hizo Wakala imejenga nyumba 861 za thamani ya kiasi cha Tshs 24,943,924,573.00 kutoka katika vyanzo vya fedha zake na imesimamia ujenzi wa nyumba 165 za thamani ya kiasi cha Tshs 15,635,012,729.80 kwa fedha iliyotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi.

Kuanzi mwaka 2011 Wakala unakusudia kuanza kutekeleza mpango wa ujenzi wa **nyumba elfu kumi (10,000)** za watumishi wa umma nchi nzima kuanzia mwaka huu 2011. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka mitano ijayo

'Tumethubutu, Tumeweza Tunazidi Kusonga Mbele'

**Karakana**
Baada ya Uhuru, Serikali imeendelea kuboresha na kujenga Karakana za Serikali kutoka Karakana nane (8) wakati wa upatikanaji wa Uhuru hadi kufikia karakana 21 ambazo zipo katika mikoa yote ya Tanzania bara zikitoa huduma ya matengenezo ya magari ya Serikali. Aidha, Mafundi na Wahandisi wa karakana hizi hususani Karakana Kuu ya M. T. Depot zilifanya kazi kubwa sana wakati wa vita kati ya nchi yetu na Uganda mwaka 1978 hadi 1979.

Wizara ya Ujenzi ilifanikisha kuandaa usajili wa magari yapatayo 21,000 ya Serikali ambayo yalikuwa yamesajiliwa kwa namba za kiraia na yalikuwa hayatambuliki kirahisi kuwa ni mali ya Serikali. Aidha, Wizara ilibuni namba za ST (magari ya Serikali Kuu), PT (magari ya jeshi la Polisi) na DFP (magari ya miradi iliyochini ya Wafadhili) kwa lengo la kusajili magari husika kulingana na majukumu yao na hivyo kuokoa fedha nyingi za Serikali.

'Tumethubutu, Tumeweza Tunazidi Kusonga Mbele'

**Vivuko**
Wakati nchi yetu inapata Uhuru mwaka 1961 hapakuwa na kivuko hata kimoja kinachojiendesha chenyewe.

Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa vivuko kama viungo muhimu kwenye barabara, iliendelea kununua na kujenga vivuko vya kutumia injini vinavyofikia 23 katika maeneo mengi ya nchi

'Tumethubutu, Tumeweza Tunazidi Kusonga Mbele'

**Mfuko wa barabara**
Mwaka 2000 Serikali ilianzisha Mfuko wa Barabara kwa ajili matengenezo ya barabara. Mfuko umekuwa kwa asilimia 741.8 kutoka shilingi billioni 40.03 mwaka 2000/2001 ulipoanzishwa hadi Shilingi billioni 296.95 mwaka 2010/2011.

**Wahandisi**
Mwaka 1961 Wahandisi wazalendo walikuwa 2 tu waliosajiliwa ambapo mwaka 2011 wamefikia 10,410.

**Makandarasi**
Kabla ya mwaka 1997 kulikuwa na jumla ya makandarasi 900. Aidha toka kuanzishwa kwake, Bodi imeweza kusajili jumla ya makandarasi zaidi ya 7,000.

**Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**
Bodi imesajili wanataaluma 527 kati ya hao 199 ni Wakadiriaji Majenzi na 328 ni Wabunifu Majengo ikilinganishwa na wataalm 10 waliokuwa wamesajiliwa hadi mwaka 1974.Vilevile yamesajiliwa makampuni 171 ya Wabunifu Majengo na 72 ya Ukadiriaji Majenzi.

## 'Tumethubutu, Tumeweza Tunazidi Kusonga Mbele'


## 9. MTANDAO WA BARABARA NCHINI

Ramani zifuatazo zinaonyesha mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa kwa kila mkoa Tanzania Bara.






ARUSHA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
ARUSHA
KEY



COAST REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY


DAR ES SALAAM REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY


DODOMA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
Dodoma
KEY



IRINGA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
Distance in km


KAGERA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY


KIGOMA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
Kigoma
KEY



KILIMANJARO REGION
TRUNK & REGIONALROAD NETWORK
KEY



LINDI REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY



MANYARA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
Distance in km


MARA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
MUSOMA
Tarime
Bunda
Mugumu
Musoma
Manyamanyama
Kangetutya
Port Ikoma
Kyabakari
Total Road Network
Total Trunk Roads
Paved Trunk Roads
Unpaved Trunk Roads
Total Regional Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
Distance in km
MOW – 2011
Sketch Map



MBEYA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY



MOROGORO REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
Morogoro
KEY



MTWARA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
Mtwara
Masasi
Mpeta
Mangaka
MOZAMBIQUE
Total Road Network
Total Trunk Roads
Paved Trunk Roads
Unpaved Trunk Roads
Total Regional Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
Distance in km
MOW – 2011
Sketch Map


MWANZA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
Total Road Network 1,534.3
Total Trunk Roads 390.0
Paved Trunk Roads 373.0
Unpaved Trunk Roads 17.0
Total Regional Roads 1,144.3
Paved Regional Roads 17.0
Unpaved Regional Roads 1,127.3
Mwanza
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Road
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
Distance in km
MOW – 2011
Sketch Map



RUKWA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY


RUVUMA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
Total Road Network 1,960.4
Total Trunk Roads 928.4
Paved Trunk Roads 192.3
Unpaved Trunk Roads 736.1
Total Regional Roads 1,032.0
Paved Regional Roads 13.0
Unpaved Regional Roads 1,019.0
Songea
Mbinga
Namtumbo
Tunduru
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
Distance in km
MOW – 2011
Sketch Map


SHINYANGA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
Bukombe
Kahama
SHINYANGA
Maswa
Kishapu
Total Road Network 1,153.6
Total Trunk Roads 656.0
Paved Trunk Roads 330.0
Unpaved Trunk Roads 326.0
Total Regional Roads 1193.0
Paved Regional Roads 11.0
Unpaved Regional Roads 1182.0
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
30 Distance in km
MOW – 2011
Sketch Map


SINGIDA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
KEY


TABORA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
TABORA
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
30 Distance in km


TANGA REGION
TRUNK & REGIONAL ROAD NETWORK
TANGA
KEY
Paved Trunk Road
Unpaved Trunk Roads
Paved Regional Roads
Unpaved Regional Roads
30 Distance in km

## 10. VIONGOZI WALIOONGOZA NAFASI YA RAIS KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 KUANZIA MWAKA 1961



**Baba wa Taifa**
Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere
Rais wa Kwanza wa Tanzania
1961 - 1985



Rais wa Awamu ya Nne kuanzia mwaka 2005, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa katika picha ya pamoja na Rais wa Awamu ya Pili (kushoto) Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi (1985 – 1995) na Rais wa Awamu ya Tatu (Kulia), Mheshimiwa Benjamin William Mkapa (1995 – 2005).

## 11. VIONGOZI WALIOONGOZA NAFASI YA MAKAMU WA RAIS KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 KUANZIA MWAKA 1961I



**Mhe. Abeid Amani Karume**
Makamu wa Kwanza
1964 - 1972



**Mhe. Aboud Jumbe**
Makamu wa Kwanza
1972 - 1984



**Mhe. Rashid Mfaume Kawawa**
Makamu wa Pili na Waziri Mkuu
1964 - 1977



**Mhe. Ali Hassan Mwinyi**
Makamu wa Kwanza
1984 - 1985



**Mhe. Jaji Mst Joseph S.Warioba**
Makamu wa Kwanza na Waziri Mkuu
1985 - 1990



**Mhe. Idrisa Abdulwakil**
Makamu wa Pili
1985 - 1990



**Mhe. Dkt. John S. Malecela**
Makamu wa Kwanza na Waziri Mkuu
1990 - 1994



**Mhe. Dkt. Salmin Amour**
Makamu wa Pili
1990 - 2000



**Mhe. Cleopa David Msuya**
Makamu wa Kwanza na Waziri Mkuu
1980-1983 & 1994 - 1995



**Mhe. Dkt. Omar Ali Juma**
Makamu wa Rais
1995 - 2002



**Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein**
Makamu wa Rais
2002 - 2010



**Mhe. Dkt. Mohammed G. Bilal**
Makamu wa Rais
Kuanzia 2010

## 12. VIONGOZI WALIOONGOZA NAFASI YA WAZIRI MKUU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 KUANZIA MWAKA 1961



Mhe. Julius Kambarage Nyerere
1961 – 1962



Mhe. Rashid Mfaume Kawawa
1962 - 1977



Mhe. Edward Moringe Sokoine
1977 - 1980
1983 - 1984



Mhe. Dkt. Salim Ahmed Salim
1984 - 1985



Mhe. Joseph Sinde Warioba
1985 - 1990



Mhe. Dkt. John Samwel Malecela
1990- 1994



Mhe. Cleopa David Msuya
1980 – 1983
1994 - 1995



Mhe. Frederick Tluway Sumaye
1995 – 2005



Mhe. Edward Ngoyai Lowassa
2005 - 2008



Mhe. Kayanza Peter Pinda
Kuanzia 2008